SportPesa
TZS. 918,137,180
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



UKURASA 5

**RAIS** Samia, WHO wamlilia Dk. Mwele, kuzikwa Dodoma




Nipashe
Jumamosi Februari 12, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580854
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

UKURASA 11

MAUAJI MENGINE MTWARA

# Mfungwa, mahabusu wauawa kwa risasi

**NI** baada ya kudaiwa kumjeruhi askari magereza...*Endelea Uk. 2*



Mkuu wa Magereza Mkoa wa Mtwara, Raymond Mwampashe.

UKURASA WA 3

## CHAMA CHA WALIMU CHATAHADHARISHA UHABA WA WALIMU

CHAMA cha Walimu Tanzania (CWT), kimesema kutokana na mwitikio mkubwa wa jamii unaotokana na mpango wa elimu bila malipo umezifanya shule

UKURASA WA 4

## MWALI ADAIWA KUMUUA BABA MKWE KWA JEMBE

MATUKIO ya mauaji yameendelea kuripotiwa nchini, safari hii mwali akidaiwa kumuua baba mkwe wake kwa kumpiga na jembe kichwani wilayani Siha

UKURASA WA 8

## MAHAKAMA KUU YABARIKI UONGOZI WA LIPUMBA CUF



MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dar es Salaam imekataa kutoa amri ya kumvua uongozi Mwenyekiti wa Chama cha Wananchi (CUF), Prof. Ibrahim Lipumba, baada ya kutupilia mbali maom-

# Watu 10 mbaroni tuhuma wizi bilioni 2.1/- kimtandao

UKURASA 2






Kamanda wa Polisi Mkoa wa Iringa, ACP Allan Bukumbi, akiwaonyesha waandishi wa habari mkoani humo jana, baadhi ya magari yanayodaiwa kununuliwa kupitia fedha za wizi zaidi ya Sh. Bilioni 2.1, mali ya kampuni ya Selcom Paytech Ltd. **Picha ndogo:** Sehemu ya fedha zilizookolewa na jeshi hilo. **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**

## Madaktari waonya matumizi ya P2

UKURASA 3

**MICHEZO** SIMBA SC, YANGA MAWINDO TOFAUTI UK.24
MAONI, KATUNI UK.6




Sehemu ya mabanda mapya ya wafanyabiashara wadogo maarufu kama machinga yakiwa yamejengwa kwa mpangilio mzuri katika soko la Ilala Mchikichini, jijini Dar es Salaam, baada ya soko hilo, kuungua moto hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mfungwa na mahabusu wauawa kwa risasi wakijaribu kutoroka

**Na Abdallah Khamis,**
MTWARA

MFUNGWA mmoja aliyekuwa akitumikia kifungo cha miaka 30 gerezani na mahabusu aliyekuwa na tuhuma za mauaji, wameuawa kwa kupigwa risasi na askari wa Jeshi la Magereza wakati wakijaribu kutoroka kwenye Gereza Kuu la Lilungu mkoani Mtwara.

Mauaji hayo yanadaiwa kutokea Desemba 17 mwaka jana majira ya saa sita mchana yakimhusisha mfungwa mwenye namba 321/2021 Juma Mohamed Mwanya na mahabusu mwenye namba ya kesi PI. 2/2020 Dionis Robat, aliyekuwa ameshtakiwa kwa kosa la mauaji katika Mahakama ya Wilaya ya Lindi.

Mkuu wa Jeshi la Magereza Mkoa wa Mtwara, Kamishna Msaidizi Raymond Mwampashe, aliiambia Nipashe jana kuwa mauaji hayo yalifanyika nje ya gereza baada ya mmoja wa waliotoroka kumshambulia kwa kitu kizito usoni askari mwenye namba B.S. 5427 Bamila Maneno.

Alidai mauaji hayo yalitokea majira ya saa sita mchana Desemba 17 mwaka jana baada ya jitihada mbalimbali za askari magereza kuwataka wahusika wajisalimishe kushindikana.

"Kwa taarifa nilizoletewa, hawa waliouawa walifanikiwa kuruka ukuta wa ngome ya magereza muda huo wa mchana na askari wetu waliposhtuka wakapiga filimbi kwa ajili ya kuwazingira lakini walishatoka nje ya gereza na kukimbilia kwenye mashamba ya korosho, hivyo jitihada za kuwatafuta zilianza mara moja kwa askari kuzunguka kila eneo huku wawili wakienda na pikipiki kuzuia barabara kuu," alidai.

Aliongeza kuwa wakati msako ukiendelea askari magereza waliokuwa na pikipiki walikutana na askari wa usalama barabarani na walipowauliza kama wamewaona wafungwa wakipita katika eneo hilo, wakawaambia wameona watu wawili wamepita wakiwa wanakimbia baada ya kuvuka barabara ya kuelekea Newala.

Alidai kuwa baada ya taarifa hiyo, askari walizunguka msitu uliokuwa karibu na eneo walioelekezwa na wakati msako ukiendelea mwenzao mmoja alipigwa na kitu kizito na mmoja wa waliotoroka huku wakimfuata askari mwenye silaha ili kumpokonya.

Mwampashe aliongeza kuwa hata walipoambiwa wajisalimishe walikataa na wakawa wanazidi kuwakabili askari ndipo walipopigwa risasi kisha wakachukuliwa kwa ajili ya kuwahishwa Hospitali ya Ligula baada ya taratibu za kipolisi katika eneo hilo kukamilika, lakini walifariki dunia baada ya kuvuja damu nyingi.

Alipoulizwa maeneo ya mwili waliyopigwa risasi, Mwampashe alidai hilo ni suala la kipolisi kwa kuwa wakati tukio linatokea hakuwapo mkoani Mtwara.

Akizungumzia tuhuma zilizowafikisha gerezani mfungwa na mahabusu waliouawa, Mwampashe alisema mahabusu alikuwa na kesi ya tuhuma za mauaji katika Wilaya ya Lindi na alihamishiwa Gereza Kuu la Lilungu Oktoba 9 mwaka jana akiwa anatumikia kifungo cha miaka miwili baada ya kujaribu kutoroka wakati akisubiri kesi yake ya mauaji iendelee huko Lindi.

"Huyu mahabusu Robart alishajaribu kutoroka katika Gereza la Nachingwea wakati akisubiri kutajwa kwa kesi yake, na alipokamatwa ndiyo akahukumiwa miaka miwili kwa kosa la kutoroka ndani ya gereza, kifungo chake kwa kosa hilo alimaliza Desemba 11 mwaka jana," alidai. Mwampashe aliendelea kudai kuwa mfungwa Mwanya aliyejaribu kutoroka alikuwa kwenye kifungo cha miaka 30 gerezani baada ya kuhukumiwa na Hakimu wa Mahakama ya Wilaya Ruangwa Julai 26 mwaka jana kutumikia adhabu hiyo alipokutwa na hatia ya unyang'anyi wa kutumia silaha.

"Huyu Mfungwa mwili wake tuliwakabidhi ndugu zake lakini mahabusu alizikwa na manispaa baada ya jitihada za kutafuta ndugu zake huko mikoa ya kanda ya ziwa kushindikana," alidai.

Mauaji hayo yametajwa kipindi ambacho serikali imeunda tume ya kuchunguza mauaji ya mfanyabiashara yanayodaiwa kufanya na baadhi ya maofisa wa Jeshi la Polisi mkoani Mtwara mwanzoni mwa mwaka huu.

# Mussa Zungu rasmi kuwa Naibu Spika

**Na Salome Kitomari,**
DODOMA

BUNGE limemchagua Mbunge wa Ilala (CCM), Mussa Zungu (70), kuwa Naibu Spika wa 13 tangu kuanza kwa muhimili huo mwaka 1961 kwa kura 296 kati ya 301 zilizopigwa.

Akitangaza matokeo hayo jana bungeni, Spika Dk. Tulia Ackson, alisema: "Kura zilizopigwa ni 301. Kati yake, 296 sawa na asilimia 98.33 zimesema ndiyo, huku tatu zikisema hapana na mbili ziliharibika. Kwa mamlaka niliyonayo namtangaza Zungu kuwa Naibu Spika."

Awali, aliomba kura na kuomba Mungu ampe imani na alipoulizwa maswali matatu ya nyongeza alirudia kuwa atafanya kwa mujibu wa Kanuni za Bunge za 2020 ambazo zimeelekeza majukumu yake pamoja na maelekezo kutoka kwa Spika.

Majibu hayo yaliwafanya wabunge hao kucheka na kumshangilia kila alipojibu.

Alipopewa nafasi ya kujieleza, Zungu alianza kutoa salamu kwa lugha ya Kiingereza kiasi cha kuwafanya wabunge wacheke huku wakimpigia makofi.

Uchaguzi huo umefanyika baada ya aliyekuwa Naibu Spika, Dk. Tulia kuchaguliwa kwa kura zote 376 kuwa Spika, baada ya aliyekuwa Spika, Job Ndugai, kujiuzulu nafasi hiyo.

Zungu amekuwa mbunge wa Ilala tangu mwaka 2005 na kabla ya uchaguzi wa jana alikuwa Mwenyekiti wa Bunge, nafasi aliyokuwa nayo kwa muda mrefu.

Pia alikuwa Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira kuanzia Januari hadi Juni, mwaka 2020.

Waliowahi kushika nafasi hiyo ni: Erasto Mang'enya (1961, 1966-1973), Frank Mfundo (1962-1964), Herman Sarwat (1964-1965), Stanslaus Kasusura (1973-1985), Austin Shaba (1986-1988), George Nhigula (1988-1990), Pius Msekwa (1990-1994).

Wengine ni Mathias Kihaule (1994-1995), Philip Marmo (1995-2000), Juma Akukweti (2000-2005), Anne Makinda (2005-2010), Ndugai (2010-2015) na Dk. Tulia (2015 hadi Februari 2022).

# Watu 10 mbaroni tuhuma wizi bil 2.1/- kwa njia ya mtandao

**Na Francis Godwin,** IRINGA

JESHI la Polisi Mkoa wa Iringa linawashikilia watu 10 akiwamo wakala wa kampuni ya Selcom Paytech Limited, Tyson Kasisi, kwa tuhuma za wizi wa zaidi ya Sh. bilioni mbili, mali ya kampuni ya Selcom Paytech Limited.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Iringa, Allan Bukumbi, aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa mtuhumiwa huyo kupitia huduma ya Selcom Pay, isivyo halali, alihamisha fedha kwenda kwenye namba mbali mbali za simu na kisha kuchukuliwa fedha taslimu kupitia wakala wa huduma za kifedha za mitandao ya simu pamoja na akaunti za benki.

"Wizi wa fedha hizo ulifanyika kwa njia ya mtandao katika mikoa ya Iringa, Dar es Salaam na Morogoro kati ya Novemba 9 na 27, 2021 baada ya wakala huyo kuchezea mfumo wa kielektroniki wa Selcom Pay unaomilikiwa na kampuni ya Selcom Paytech Limited," alisema.

Kamanda Bukumbi alisema wakala huyo kwa njia ya udanganyifu alianza kujitumia fedha pamoja na kuwatumia watu wengine na kwa kushirikiana na genge la uhalifu, hivyo kuiba Sh. 2,129,856,000.

Hata hivyo, Bukumbi alisema polisi wamekamata Sh. 956,974,000 kutoka kwa watuhumiwa na washirika wa uhalifu huo ambao walipokea sehemu ya fedha hizo na kuzificha katika maeneo mbalimbali yakiwamo ya makazi na mashambani.

Bukumbi pia alisema Sh. 121,215,783 zimezuiwa katika moja ya benki za kibiashara mkoani Iringa zikiwa zimetokana na zao la uhalifu.

Alisema upelelezi uliofanywa hadi sasa umebaini kuwa genge hilo la uhalifu na wizi wa fedha za kampuni hiyo, uliongozwa na watu watatu ambao ni Kasisi, Patrick Chalamila na Evarist Chalamila ambao wamebainika kuwa ni wanufaika wakuu wa uhalifu huo .

Mbali na fedha hizo kukamatwa, pia alisema mali zinazosadikika kuwa za uhalifu zimekamatwa na kuhifadhiwa yakiwamo magari manne yenye thamani ya Sh. milioni 303.

Kamanda Bukumbi alitaja magari hayo kuwa ni Scania yenye jina la Patrick Chalamila lenye thamani ya Sh. milioni 128, Mitsubishi Fuso yenye usajili namba T 796 DXV yenye jina la Kasisi likiwa ni thamani ya Sh. milioni 75, gari aina ya Toyota Harrier namba T 719 DXX lenye jina la Kasisi likiwa na thamani ya Sh. milioni 72 na gari aina ya Nissan Juke lenye usajili T 605 DXV la Patrick Chalamila lenye thamani ya Sh. milioni 28.

Licha ya magari hayo, Bukumbi alisema Jeshi la Polisi limekamata gari aina ya Toyota IST lenye namba za usajili T 576 DRN mali ya Patrick Chalamila lililotumika kufanikisha uhalifu kwa kusafirisha fedha za wizi kutoka Madibira wilayani Mbarali na Ilula wilaya ya Kilolo kwenda kuzificha Kilombero mkoani Morogoro.

Kamanda alisema ushahidi uliokusanywa hadi sasa umetosha kuwafikisha watuhumiwa 10 mahakamani kujibu tuhuma zinazowakabili za kuongoza genge la uhalifu na kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu .

HABARI KITAIFA



Mkufunzi kutoka Idara ya Masomo ya Kompyuta ya Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), Sakina Msonde, akizungumza wakati wa semina kuhusu elimu kwa wanafunzi wa kike wanaosoma masomo ya sayansi ili kuwajengea uwezo wa kiuchumi, iliyofanyika katika Ofisi za Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Madaktari waonya matumizi ya P2

**Na Romana Mallya**

RAIS wa Chama cha Madaktari Tanzania (MAT), Dk. Shadrack Mwaibambe, amekemea vijana dhidi ya matumizi holela ya vidonge vya kuzuia mimba (P2) ambavyo vina athari katika homoni zao na uwezekano wa baadaye kupata matatizo ya uzazi.

Kauli hiyo inakuja baada ya juzi Kamati ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI, kubainisha ongezeko la matumizi ya vidonge hivyo hasa kwa wasichana wenye umri unaoanzia miaka 14 hadi 24.

Akizungumza na Nipashe jana mkoani Dar es Salaam, Dk. Mwaibambe, alisema matumizi holela ya vidonge hivyo huchangia kuharibu mzunguko wa mwezi wa mwanamke. "Matumizi ya muda mrefu siyo salama kwao, usalama wao hasa kwa umri huo uliotajwa ni kukwepa kujihusisha na vitendo vya ngono mpaka umri utakapofika na hata ukifika wasifanye ngono zembe.

"Ni rahisi kupita kwenye maduka ya dawa na kugundua matumizi ya vidonge hivi yameongezeka lakini ni vigumu kuthibitisha utoaji wa mimba.

"Hawa wanaotumia P2 wanaonekana ni wajanja wana elimu hiyo lakini lipo kundi kubwa tu halina elimu ya P2, maana yake hili linakwenda sambamba na utoaji mimba," alisema.

Alishauri kama kamati imepitia kwenye P2, iende mbali zaidi iangalie na utoaji mimba holela ambao ni mbaya zaidi na unaathiri kizazi. "P2 inaathiri homoni na matumizi ya mara kwa mara ni hatari kwa sababu ule mzunguko wa hedhi wapo wanaoolewa na umri wa miaka 24, ukizoea vidonge hivi mzunguko wako unaweza kupata athari hata yale matumizi ya kalenda unaweza kushindwa kufuata, unafanya mzunguko haueleweki," alifafanua.

Dk. Mwaibambe alisema mtoto wa miaka 14 kuuziwa vidonge hivyo, kunamaanisha kuna uuzaji holela wa dawa hizo.

"Wito wangu kwa wanaume, miaka 14 ni mtoto hata maumbile hayajakomaa, wanaume tuwaonee huruma hawa watoto na tuende mbali zaidi, hawa ni watoto wetu, wengine ni wadogo zetu ni taifa la kesho, ni walimu ni wauguzi, ni madaktari ni wanasheria wa kesho.

"Viungo havijakomaa, hapa ni kuwarubuni na mara nyingi unakuta wanafanya ngono na watu waliopevuka waliowazidi umri, mtoto wa miaka 14 unampa mimba viungo havijakomaa, inakuwa ni mtoto anazaa mtoto na unamhatarishia maisha yake," alisema.

Dk. Mwaibambe alihoji inakuaje mtoto mwenye umri wa miaka 14 anauziwa dawa hizo.

"Ninashauri elimu ya uzazi ishuke zaidi kuanzia darasa la tano na kuwe na mada za mara kwa mara shuleni zinazozungumzia elimu ya uzazi. Ustawi wa jamii hii ndiyo jamii yenyewe, siyo kukaa ofisini lazima kuwapo ubunifu vitendo ambavyo vinaharibu taifa vifanyiwe kazi," alisema.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti wa kamati hiyo ya Bunge, Fatma Tawfiq, licha ya kuwa na lengo la kuzuia mimba ila matumizi ya vidonge hivyo ambavyo huuzwa kwa bei ya chini yamekuwa yakichochea maambukizi ya Virusi vya UKIMWI (VVU).

Alisema hilo linaonyesha wasichana wanaogopa zaidi mimba kuliko VVU ndiyo maana wanatumia P2 kama njia ya kuzuia mimba na kuacha kutumia kondomu ambazo zinawakinga dhidi ya maambukizi ya VVU, magonjwa ya ngono na mimba zisizotarajiwa.

# CWT yatahadharisha uhaba wa walimu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

CHAMA cha Walimu Tanzania (CWT), kimesema kutokana na mwitikio mkubwa wa jamii unaotokana na mpango wa elimu bila malipo umezifanya shule nyingi kuwa na uhaba wa walimu.

Aidha, kimeomba serikali kulipa madai mbalimbali ya walimu ambayo bado yapo kwenye Halmashauri ili kuongeza ari ya kutekeleza wajibu wao kwa ufanisi.

Katibu Mkuu wa CWT, Deus Seif, alitoa tahadhari hiyo jana kwenye Hafla ya Utoaji wa Tuzo za Ubora wa Taaluma kwa matokeo ya mtihani wa kumaliza Elimu ya Msingi, Kidato cha Nne na Kidato cha Sita kwa mwaka 2021.

Aliomba serikali kutoa ajira kwa wananchi nchini ili kuwasaidia watoto ambao tayari wana vyumba , madawati na vitabu.

Pia aliomba kujengwa kwa nyumba za walimu hasa wa maeneo ya pembezoni ambapo kuna shida zaidi ya nyumba hata za kupanga.

"Pia kuna madai mbalimbali ya walimu bado yapo katika Halmashauri zetu na hata Wizarani, likizo, matibabu, uhamisho, malimbikizo ya mishahara, madaraja, masomo tunaomba uhakiki wa mara kwa mara ufanyike na walimu walipwe ili kuongeza ari ya kufanya kazi,"alisema.

Akizungumza katika hafla hiyo akimwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, alisema hadi sasa serikali imetoa Sh. trilioni 1.43 kwa ajili ya kugharamia Mpango wa Elimu Msingi Bila Malipo.

Bashungwa alisema mpango huo umeleta fursa ya upatikanaji wa elimu kwa kuongeza uandikishaji wa wanafunzi, kutokana na kuondolewa kwa vikwazo.

Alisema katika mwaka 2016, jumla ya wanafunzi 2,670,125 waliandikishwa, kati ya hao wanafunzi 917,137 wa elimu ya awali, 1,386,592 wa darasa la kwanza na wanafunzi 366,396 wa kidato cha kwanza.

# LHRC: Maboresho Sheria ya Habari yawe shirikishi

**Na Christina Mwakangale**

KITUO cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), kimesema kwamba baada ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kufungua mlango wa majadiliano na wadau wa habari, ni muhimu mchakato wa maboresho ya Sheria ya Huduma ya Vyombo vya Habari, 2016, ushirikishe wadau hao.

Pia kimesema serikali ijikite katika mapitio ya sheria zote zinazogusa sekta ya habari ili kuboresha mazingira ya upatikanaji wa taarifa nchini ambayo ni haki ya kila mwananchi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo hicho, Anna Henga, aliyasema hayo jana mkoani Dar es Salaam, wakati akizungumza na waandishi wa habari kupongeza hatua ya serikali kuyafungulia magazeti manne yaliyofungiwa.

Anna alisema ili kuweka mazingira rafiki na kurejesha hali ya uchumi wa vyombo vya habari viliivyoathirika na sheria hizo, alisema wizara ifuate hatua ya maboresho ya sheria za habari ili kuondoa tatizo hilo ambalo huvikumba mara kadhaa vyombo vya habari nchini.

Nape alitoa tamko wakati wa semina na wahariri, Februari 10, mwaka huu, ikiwa ni kiashiria kizuri cha kurudi kwa uhuru wa vyombo vya habari, na ni muda mwafaka sasa kuangalia changamoto za kiujumla za sheria zinazoikabili sekta ya habari na uhuru wa kujieleza.

"Mtakumbuka kwamba Aprili 6, mwaka huu, Rais Samia Suluhu Hassan wakati anaapisha safu ya makatibu na manaibu wakuu, wakuu wa taasisi za serikali alitoa agizo kwa iliyokuwa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kufungulia vyombo vya habari."

"Juni 28, 2021 wakati wa mkutano kati ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na Jukwaa la Wahariri Tanzania kuhusu siku 100 za uongozi wake, alitoa agizo la kuweka mazingira mazuri kwa vyombo vya habari kwa kuwa hali haikuwa nzuri."

Akifafanua zaidi, Anna alisema kituo hicho ni sehemu ya wadau wa sheria za habari, tangu utungaji wa sheria ulipoanza na kilibaini baadhi zinakwamisha urahisi wa upatikanaji wa taarifa kwa jamii.

Alisema miongoni mwake ni Sheria ya Makosa ya Mtandao, 2015; Sheria ya Upatikanaji wa Habari, 2016; Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano pamoja na kanuni zake na Sheria ya Huduma ya Vyombo vya Habari, 2016.

"Ni ukweli kwamba, sheria hizi bado zipo na zinaendelea kuminza haki ya kupata taarifa kama ilivyoainishwa katika Ibara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977, imeathiri magazeti, redio, televisheni, mitandao ya kijamii na uhuru wa intaneti.

"Kikosi kazi kitakachoundwa na waziri kupitia upya na kutekeleza uamuzi wa Mahakama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu Sheria ya Huduma ya Vyombo vya Habari, 2016, wadau watoe maoni ya kina yatayochangia kuboreshwa kwa sheria za habari," alisema.


**Death and Funeral Announcement**

As His Decree is Issued, so is His Command obeyed.
Those who are sent, come, O Nanak; when they are called back, they depart and go.||1||



**Kuldip Singh Grewal**

**1977 - 2022**

It is with a heavy heart that the Grewal Family Announces the untimely sad demise of Kuldip Singh Grewal, Director of Jubilee Tyres (2000) Ltd & Grewals Transport Ltd, in a road accident between Dodoma and Babati on 7th February 2022

Son of Late Tarlochan S. Grewal and Sarjit K. Grewal
Husband to Gagandeep K. Grewal
Father to Rajvir and Harmeet
Brother to Dilvinder, Dipu, Nicky, Aneet, Teji and Shilu
Brother-in-law to Sukhbir and Simran
Uncle to Jasveen, Jai, Anayk, Savjyot, Sahib, Gaganraj, Pari, Mannat and Mahek

**Saturday 12th February 2022**
Grewal Residence, Themi Hill, Arusha: **1:00 pm** to **2:30 pm**
Hindu/Sikh Cremotorium: **2:30 pm**, Esso Area Arusha

***"Kuldip you will be missed by all brothers, sisters, relatives and friends"***
**May the Almighty rest the departed soul in eternal peace**

*Much appreciated by the Grewal Family, Mangat Family & Sohal Family*

**Family Contact**
Dipu: +255 784 420220 / Raji: +255 754 287700

Due to *Covid-19* restrictions, please attend the Funeral with Appropriate PPE

**WAHEGURU - WAHEGURU - WAHEGURU**

216702702



Mkuu wa Wilaya Ilemela, mkoani Mwanza, Hassan Masala (wa pili kushoto), akikabidhi cheti kwa mmoja wa askari waliofanya vizuri katika kupambana na matukio mbalimbali ya uharifu, likiwemo la mauja ya watu watatu wa familia moja pamoja na dereva Taxi anayedaiwa kuuawa Januari 26 mwaka huu na abiria walio mkodi ambao ni mtu na mkewe, katika hafla fupi ya kuwapongeza, iliyondaliwa na Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mwanza, Ramadhan Ng'anzi (kushoto). **PICHA: ROSE JACOB**

# Saratani tano Kanda ya Ziwa zatajwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Afya imetaja saratani tano zinazoongoza Kanda ya Ziwa ikiwamo ya kibofu cha mkojo huku ikibainisha kuwa bado inafanya utafiti ili kubaini chanzo chake.

Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, alisema hayo bungeni jana alipokuwa ikijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Kabula Shitobela.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji serikali imefikia wapi kuhusu kufanya uchunguzi ili kujua chanzo cha ugonjwa wa saratani katika mkoa wa Mwanza na Kanda ya Ziwa, kwa Kuwa unaongoza kuwa na wagonjwa wengi.

"sJe, kuna Mpango gani wa kudhibiti ongezeko la ugonjwa huo?" alihoji Mbunge huyo. .

Katika majibu ya swali hilo, naibu Waziri alisema serikali kupitia wizara imeshafanya utafiti wa kina nchi nzima uliosaidia kutambua kuwa Kanda ya Ziwa ni saratani zipi zinaongoza.

Alitaja saratani hizo kuwa ni za kibofu cha mkojo, mji wa uzazi wa kinamama, saratani ya damu, macho na figo.

Pia alibainisha kuwa kuwa wataalamu wamekusanya sampuli 7,000 za damu za watu ambao hawana saratani ili kulinganisha na sampuli za damu za wenye saratani.

Alisema utafiti huo utasaidia kubaini chanzo cha hizo saratani kwa kuwa hadi sasa bado utafiti unaendelea na visababishi vinavyosemwa bado ni nadharia tu kutokana na shughuli za kijamii katika maeneo husika.

Hadi sasa, alisema mpango wa kudhibiti ongezeko umejikita katika kutoa elimu ya afya kwa viashiria vinavyodhaniwa, pamoja na kuzingatia Mkakati wa kitaifa wenye maeneo saba yaliyoainishwa ili kudhibiti viashiria vya saratani.

# Mwali adaiwa kumuua Baba mkwe kwa jembe

**Na Anjela Mhando,** SIHA

MATUKIO ya mauaji yameendelea kuripotiwa nchini, safari hii mwali akidaiwa kumuua baba mkwe wake kwa kumpiga na jembe kichwani wilayani Siha mkoani Kilimanjaro.

Jana Mkuu wa Wilaya ya Siha na Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, Thomas Apson, alithibitisha kupokea taarifa kuhusu mauaji hayo yaliyotokea katika Kijiji cha Mlangoni, Kata ya Garagua.

"Ni kweli hayo mauaji yalitokea jana (juzi) jioni baada ya Joyce Siao (45), ambaye ni mke wa mtoto wa mzee Godson Moshi (80), kumpiga jembe kichwani baba mkwe wake huyo.

"Kama Mkuu wa Wilaya, nasisitiza familia zenye ndugu au wakazi ambao ni wagonjwa wa akili ni vyema wakapelekwa katika Hospitali ya Wilaya kwa uchunguzi zaidi na kupatiwa tiba. Nasema hivi kwa sababu nimeambiwa huyo mwali alikuwa mgonjwa wa akili,"alisema.

Alipotafutwa na Nipashe kuzungumzia tukio hilo, Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Mlangoni, Swalehe Mohamed, alisema lilitokea juzi majira ya saa 1:30 jioni nyumbani kwao.

"Huyu mwali (Joyce) alikuwa akiishi na baba mkwe wake (Godson) baada ya mume wake kufariki dunia miaka kadhaa iliyopita. Kabla ya kuchukua uamuzi wa kumpiga na jembe kichwani, mtuhumiwa wa mauaji hayo alikuwa amehitilafiana na baba mkwe wake.

"Sasa baada ya kutekeleza dhamira yake, majirani walisikia kelele na kukimbilia katika nyumba hiyo na kumkuta baba mkwe wake akiwa ameanguka. Walimchukua baba huyo na kumpeleka hospitali ya wilaya kwa ajili ya kupatiwa matibabu, lakini kabla ya kupatiwa matibabu, alifariki dunia," alidai.

Diwani wa Garagua (CCM), Zakaria Lukumay, alipoulizwa kuhusu mauaji hayo, alisema alipokea taarifa hiyo jana na tayari mtuhumiwa wa mauaji hayo amekamatwa na anashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa mahojiano zaidi.

Juzi wilayani Moshi mkoani humo, watu wengine watatu ambao ni ndugu wa familia moja, waliuawa kikatili na wawili kati yao miili yao kuteketezwa kwa moto katika Kijiji cha Manushi Ndoo, Kata ya Kibosho Magharibi.

# TMDA yawapa msaada watoto wenye ulemavu

**Na Salome Mwasamale**

MAMLAKA ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) imekabidhi msaada wa taulo za kike wenye thamani ya Sh. milioni saba kwa taasisi ya watu wenye ulemavu ya Disabilities Community Development Organisation (DCDO) ili kufanikisha mradi wao wa hedhi salama kwa watoto wenye ulemavu.

Akikabidhi msaada huo jana, Meneja Mawasiliano na Elimu kwa Umma wa (TMDA), Gaudensia Simwanza, aliwataka viongozi na wanachama wa taasisi hiyo kuhakikisha mradi huo unatumika kwa lengo lililokusudiwa na kuwafikia watoto hao kwa wakati.

"Tunaomba mjitahidi msaada huu uwafikie walengwa kama vile mlivyokusudia kwa kuwa tumeshuhudia baadhi ya taasisi zikipokea misaada na badala yake kutumia kwa lengo lingine ambalo halikukusudiwa, hivyo naomba ninyi msiige mfano huo ambao hauwafurahishi wanadamu na Mungu pia,"alisema.

Aliwapongeza kwa uamuzi wa kulisaidia kundi maalumu la watu wenye ulemavu kwa kuwa linahitaji msaada huo kutokana na hali zao za kiuchumi kuwa duni.

Meneja huyo alisema TMDA iko tayari kuendelea kushirikiana na DCDO katika kuhakikisha mradi huo na miradi mingine itakayoandaliwa inafanya vizuri na kuigusa jamii moja kwa moja.

Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Kinondoni, James Mgego, aliyataka mashirika na jamii kwa ujumla kujitokeza kuunga mkono jitihada zinazofanywa na DCDO za kuwasaidia watu wenye ulemavu kwa kuwa wanahitaji msaada kutoka kwa jamii.

"Kusaidia watu wenye mahitaji maalumu ni ibada, hivyo naisihi jamii iache kutumia fedha zao kwa matumizi yasiyompendeza Mungu badala yake iamue kuelekeza nguvu kwa makundi haya maalumu ambayo yanahitaji msaada wetu kama walivyofanya DCDO," alisema.

Akizungumza mara baada ya kupokea msaada huo, Katibu Mkuu wa DCDO, Mwalimu Iddi Mshindo, aliishukuru TMD na kuahidi kuzifikisha taulo hizo kwa walengwa kama ilivyokusudiwa.

Alisema kuwa baada ya kupokea msaada huo hatua inayofuata ni kuandika barua kwa baadhi ya shule wanazotarajia kukabidhi msaada huo ili kupewa ruhusa na siku inayofaa na baada ya kupokea majibu, wataanza kugawa Taulo hizo.

"Tunaishukuru sana TMDA kwa kukubali ombi letu la kutupatia taulo kwa ajili ya watoto wenye ulemavu wanaosoma katika shule mbalimbali nchini. Tunaahidi zitafika kwa kuwa hiyo ndiyo kiu yetu kuhakikisha watoto hao wanapata huduma hiyo kutoka kwetu," alisema.

Aliziomba mamlaka na taasisi nyingine kujitokeza kuunga mkono jitihada zao kuwasaidia watu wenye ulemavu, hasa wanafunzi ili watimize ndoto zao kielimu.

Alisema mradi huo umelenga kufanyika nchi nzima lakini kwa kuanzia wanatarajia kuutekeleza katika mikoa mitatu ya Dar es Salaam, Pwani na Tanga.

# Mtoto auawa na kuwekwa ndani ya sandarusi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

PENDO Athumani (3), mkazi wa kata ya Nyihogo Manispaa ya Kahama, amekutwa ameuawa na watu wasiojulikana na mwili wake kufungwa katika mfuko wa sandarusi na kutupwa nyuma ya nyumba aliyokuwa akiishi na mama yake mzazi.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Nyihogo, Idd Mitimingi, alibainisha hayo jana wakati akizungumza na gazeti hili ofisini kwake kuhusiana na mauaji hayo ambayo yalitokea Februari 9, mwaka huu. Alisema mtoto huyo aliokotwa akiwa amekufa siku moja baada ya kupotea na kwamba mzazi wake alikuwa akiendelea kumtafuta.

Mitimingi alisema, awali alipatiwa taarifa za kupotea kwa mtoto huyo kabla ya kupatikana akiwa amefariki dunia na baada ya kukagua mwili huo ulionyesha dalili za kunyongwa.

"Mtoto bado mdogo na alikuwa bado anahitaji malezi ya baba na mama. Alipotea katika mazingira ya kutatanisha kwa mujibu wa mama yake mzazi lakini amepatikana akiwa amekufa tena kwa kufungwa kwenye sandurusi na kutupwa nyuma ya nyumba aliyokuwa akiishi," alisema Mitimingi. Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Joseph Paulo, alithibitisha kutokea mauaji hayo na kwamba mtoto huyo alinyongwa na watu wasiojulikana na kutupwa.

Alisema upelelezi wa tukio hilo unaendelea ili kuwabaini wahusika waweze kufikishwa katika vyombo vya sheria.

# Samia, WHO wamlilia Dk. Mwele Malecela, kuzikwa kwao Dodoma

**Na Romana Mallya**

Rais Samia Suluhu Hassan na Shirika la Afya Duniani (WHO) wamemlilia aliyekuwa Mkurugenzi wa Magonjwa Yasiyopewa Kipaumbele katika shirika hilo, Dk. Mwele Malecela (58), ayefariki dunia juzi Geneva, Uswisi.

Mwele kabla ya nafasi hiyo alikuwa Mkurugenzi wa Vituo vya Kudhibiti magonjwa ndani ya shirika hilo, Kanda ya Afrika. Pia aliwahi kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) hadi Desemba 17, 2016.

Katika ukurasa wake wa Twitter juzi, Rais Samia alisema: "Nimesikitishwa sana na kifo cha Dk. Mwele Ntuli, mwana wa Afrika ambaye ameitumikia vyema Tanzania ndani na nje ya mipaka.

"Pole zangu zimfikie John Malecela na familia yake yote wakati huu wa majonzi mazito. Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi. Amina."

Naye Mkurugenzi wa WHO Kanda ya Afrika, Dk. Matshidiso Moeti, katika taarifa yake jana alisema amehuzunishwa na kifo chake.

Alisema kabla ya nafasi yake ya sasa mwaka 2017 hadi mwishoni mwa 2018 alifanya kazi kama mkurugenzi katika ofisi ya WHO Kanda ya Afrika.

"Dk. Mwele ametambulika na kuheshimika duniani kama mwanasayansi na mtafiti. Mchango wake mkubwa kwa kazi za WHO Afrika haupimiki. Agenda ya maboresho ya mifumo yetu ilifaidi mchango wa maono yake, mawazo na bidii katika kuandaa mipango mikakati, utekelezaji, uhusishaji wa wadau, uhamasishaji wa rasilimali na uandishi wa matokeo," alisema.

Alisema Dk. Mwele alitoa mchango mkubwa katika kuandaa mpango wa Mafunzo ya Uongozi ambao sasa

unatoholewa na ofisi za WHO za mabara mengine na unatumika kujenga uwezo wa viongozi wa sekta ya afya ngazi za kitaifa duniani kote.

"Alitoa mchango wa maana kufanikisha mipango mahsusi ya kazi zetu, alikuwa kinara kwenye juhudi zetu kuwafikia wadau na wafadhili wa kazi zetu.

Hulka yake ilibeba tunu za WHO za kuthamiana na kujenga uaminifu.

"Alifanya uamuzi wake akizingatia mapendekezo husika ya kisayansi na ushahidi. Udhati wake haukuyumba na ndivyo ilivyokuwa pia kwa uwezo wake mkubwa kushirikiana na wenzake na wadau wengine.

Alisema alikuwa mtu anayewajali na kuthamini wafanyakazi wenzake kama watu muhimu na aliwekeza muda na juhudi kuwawezesha kwa mambo makubwa na madogo.

"Hapakuwa na swali kwenye mwelekeo wake wa dhati. Siku zote tutaenzi na kumkumbuka kama mwenzetu, rafiki na mtetezi wa walio pembezoni

katika jamii zetu na katika nchi zetu," alisema.

Naye Mkurugenzi Mkuu NIMR, Prof. Yunus Mgaya, alisema Dk. Mwele alifanya kazi NIMR kuanzia mwaka 1987 hadi mwaka 2016 akipanda kutoka mtafiti kijana hadi mbobezi na baadaye Mkuu wa idara hadi Mkurugenzi wa Utafiti na mwaka 2010 aliteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu akiwa mwanamke wa kwanza kushika nafasi hiyo.

Prof. Mgaya alisema kwa kipindi chote akifanya kazi NIMR alishughulika na utafiti wa ugonjwa wa matende na mabusha unaosababishwa na mbu aina ya Culex.

"Utafiti wake ulipamba alipomaliza PhD mwaka 1995 katika Chuo Kikuu huko London, ilihusu mambo hayo ya matende na mabusha. Aliamini kupitia utafiti kutasaidia kutokomeza magonjwa haya. Jitihada zake zilitambulika kimataifa.

"Alikuwa balozi wetu wa kimataifa na alitupa heshima kwamba kumbe Watanzania tunaweza na wanawake wanaweza, huu ni msiba mkubwa tumepoteza mtu ambaye alikuwa kiungo kwetu na dunia hasa magonjwa yasiyopewa kipaumbele.

**MZEE MALECELA**

Baba wa marehemu, Mzee Malecela alisema Dk. Mwele alikuwa anaugua huko Uswizi kwa muda mrefu akisumbuliwa na matatizo ya nyongo na mengine.

"Jana (Juzi) saa 12:30 jioni ndiyo nikapata simu kuwa ameaga dunia, Mwele ni mzaliwa wa kwanza kama familia tulimpenda sana na alitupenda, alipenda ushirikiano na wenzake. "Ila kama ilivyo kwenye vitabu vya dini iwe Qurani Tukufu, Biblia vinasema tumekuja hapa kwa mapenzi yake na tunaondoka hapa kwa mapenzi yake, ninawaomba watanzania muungane nami kumwombea."

Mzee Malecela alisema Mwele alikuwa mtoto anayependa wenzake na kwa wale waliosoma naye na kufanya kazi pamoja watakubaliana kuwa alipenda kazi.

**MAZISHI**

Mzee Malecela alisema kwa sasa ni mapema kusema utaratibu wa mazishi lakini ratiba itakapopangwa atazikwa kijijini kwao Dodoma. Mwaka 2015 katika Uchaguzi Mkuu, Dk. Mwele alikuwa miongoni mwa waliochukua fomu kugombea kiti cha urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM).


WOMEN FUND TANZANIA TRUST
Empowering Local Women Heroes

**THE REGISTERED TRUSTEES OF WOMEN FUND TANZANIA (WFT TRUST)**

**WITO WA MAOMBI YA KUTEKELEZA MIRADI KUENDELEZA HAKI ZA WANAWAKE, WASICHANA NA WATOTO TANZANIA KWA MWAKA 2022.**

The Registered Trustees of Women Fund Tanzania (WFT Trust) ni Mfuko wa kwanza wa uwezeshaji wa kutetea haki za wanawake ulioanzishwa kwa ajili ya wanawake, wasichana, na watoto. Mfuko huu unatazamia kufikia kwa jamii yenye usawa na haki kwa kuondoa sababu zinazopelekea mgawanyo usio sawa wa mamlaka, ikiwa ni pamoja na ukosefu wa usawa wa kijinsia, na mifumo mingine kandamizi, mitazamo hasi ya kijamii katika nyanja mbalimbali. WFT Trust inafanya hivi kwa kutoa ufadhili wa Mashirika yanayofanya utetezi wa haki za wanawake, wasichana, na watoto pamoja na mashirika ya kutetea haki za kijamii ili kuweza kukuza sauti na kuleta mabadiliko ya pamoja ili kuwa na mabadiliko endelevu ya kijamii.

Lengo kuu la WFT Trust ni kufadhili Mashirika yanayotetea Haki za Wanawake na Tapo la Wanawake, haswa katika ngazi ya jamii.
WFT Trust inaamini na kuwekeza katika TAPO la wanawake wanaotetea ufeminia unaotokana na ushiriki wa majukwaa tofauti, uzoefu, na michakato mbali mbali inayotumia maarifa, ujuzi wa mashirika, vikundi, watu binafsi na wanaharakati wanaofanya kazi ndani ya Tanzania.

**Nani anaweza kutuma maombi**
WFT Trust inapokea maombi kutoka kwa taasisi za kisheria (Wanawake, wasichana na watoto, mashirika ya haki za wanawake yanayoongozwa na wanawake, mashirika ya kijamii, vikundi, taasisi na mashirika yanayoongozwa na wanaume yanayofanya kazi kimageuzi na kuendeleza ajenda ya utetezi wa haki za wanawake) yaliyo ndani ya Tanzania. Kwa habari zaidi tafadhali tembelea tovuti yetu: www.wft.or.tz

**Maeneo muhimu ya ufadhili katika 2022 ni:**

1. **Ukatili dhidi ya wanawake, wasichana na watoto** - unaolenga kushughulikia Rushwa ya Ngono, Mauaji ya Wanawake, Unyanyasaji wa Kijinsia Mtandaoni, ukatili unaohusiana na afya ya akili kwa wanawake, wasichana, watoto pamoja na makundi mengine ya kijamii yaliyo pembezoni na wale walioathiriwa na mila/tamaduni kandamizi. Hii pia inajumuisha haki za kielimu - inayolenga kuondoa kwa masuala yanayopelekea kuzuia usawa kwa wasichana kushiriki na kupata elimu ikijumuisha masuala ya ubakaji, mimba na ndoa za utotoni, na mipango ya kusaidia msichana kuingia tena katika mifumo rasmi ya shule.

2. **Ushiriki wa Kisiasa na Uongozi wa Wanawake** - kushughulikia masuala yaliyopo na ambayo yanazuia wanawake na wasichana kushiriki kikamilifu katika michakato ya uchaguzi ikiwa ni pamoja na mifumo yenye changamoto na miundo inayowazuia wanawake na wasichana kuingia na kusalia katika nafasi za uongozi katika jumuiya zao, mashirika, na maeneo mengine ya umma.

3. **Haki ya Uchumi Endelevu** - kuvunja vizuizi vya kisera na kitamaduni ambavyo vinapunguza ushiriki wa wanawake na wasichana kiuchumi na kuwazuia kufaidika na sekta pana za kiuchumi kama vile mafuta, gesi na shughuli za uchimbaji. Hii pia inajumuisha ushiriki katika mikakati mipana ya sera inayolenga kukuza sauti ya wanawake na wasichana katika mipango ya bajeti ya kijinsia, huduma za ujumuishaji wa kifedha, utoaji wa msaada wa wanawake kama vile elimu ya Wanawake na Pesa, na zingine.

4. **Haki ya Mazingira -** kushughulikia sera, sheria, na changamoto za kitamaduni zinazowakabili wanawake na wasichana wanaopaza sauti zao ikiwa ni pamoja na kushughulikia athari mbaya za uharibifu wa mazingira kwa kuzingatia mabadiliko ya hali ya hewa na haki ya ardhi kwa wanawake, wasichana na wengine pamoja na makundi yaliyo pembezoni.

5. **Utafiti na Uhifadhi wa Taarifa za Kifeminia** - Kutumia mrengo wa ufeminia kuimarisha utafiti wa ufeminia kwenye maeneo mbalimbali kama vile usalama wa wanawake wanaofanya kazi kutatua migogoro na kushiriki kwenye michakato ya kuleta amani, kuweka kumbukumbu za wanawake kwa kutumia fasihi, picha na video zinazohoji masuala ya usawa wa kijinsia pamoja na mifumo kandamizi. Waombaji pia wanaweza kuzingatia mada tofauti kama vile kuonyesha michango ya wanawake na wasichana kupitia ke-storia kuendesha mijadala, matumizi ya ubunifu ya majukwaa na vyombo mbalimbali na programu za redio za jamii.

6. **Michezo, sanaa na tamaduni** - Kuendesha shughuli zinazolenga kupinga vitendo vya kutengwa kwa misingi ya kijinsia na unyonyaji, upendeleo ikiwa ni pamoja na lugha ya kudhalilisha kwa ajili ya kubadilisha sera, sheria, kanuni za kijamii katika michezo, sanaa, utamaduni na nyingine zinazohusiana na hizo ambazo zinapelekea udhalilishaji na kuondoa utu na staha ya mwanamke na msichana katika jamii.

7. **Masuala ya Haki ya Afya ya Uzazi** - Maombi yako wazi kwa ajili ya kutekeleza shughuli zinazolenga kukuza uelewa wa haki pamoja na masuala mtambuka ya afya ya uzazi kwa wanawake na hatua za kusaidia harakati za utetezi unaojikita katika kushughulikia maswala yanayowanyima wanawake na wasichana kufanya maamuzi ya msingi na yanazozingatia ufeminia na kushughulikia haki ya uzazi kwa ajili ya ujenzi wa harakati za kijamii zinazoboresha uwezo wa wahusika wakuu kutetea na kurahisisha upatikanaji wa taarifa muhimu za haki ya afya ya Uzazi, ikiwa ni pamoja na huduma, kufanya maamuzi sahihi, ushiriki na kuwawezesha kutekeleza mikakati ya kuimarisha upatikanaji wa haki za afya ya uzazi kwa makundi yaliyo pembezoni ikiwa ni pamoja na walemavu na makundi mengine.

8. **Kujenga vuguvugu la kiharakati la kuleta pamoja wanawake na wasichana kimkakati na kuimarisha TAPO la wanawake Tanzania** - Kutekeleza shughuli mbalimbali za kukuza njia za makutano katika kuharakisha mabadiliko ya ndani ya harakati za wanawake na harakati zingine za kijamii pamoja na zile zinazofanya kazi kuendeleza haki za walemavu, haki za watoto, haki za afya ya uzazi, haki za wahamiaji na haki ya mazingira kwa hatua za pamoja na utekelezaji wa pamoja. Kuimarisha harakati za kubadilisha mifumo, sera, na mitizamo ya kijinsia katika tamaduni, kanuni za kijamii, na pia katika mifumo ya sera na sheria katika viwango tofauti.

**Madirisha kwa Ajili ya Maombi ya Ufadhili:**

**1. DIRISHA NDOGO**
Dirisha hili ni kwa ajili ya asasi na mashirika ya kijamii ya kutetea haki za wanawake, wasichana na watoto, na vikundi vya wanaharakati vilivyosajiliwa walio katika maeneo ya vijijini na mijini. Dirisha hili linafunguliwa pia kwa vikundi vya jamii yanayoanza, na yenye nia ya kujenga uwezo wao wa kiuendeshaji na wa kukuza uhamasishaji unaopelekea kukuza haki za wanawake, wasichana, na watoto katika jamii zao
- Muda wa utekelezaji ni kati ya miezi 0 na 3
- Shughuli zinazolenga kutoa sauti kwa masuala ya wanawake na wasichana, hasa wanawake waliotengwa, makundi maalum na watu wanaoishi katika mazingira magumu katika jumuiya za mitaa.
- Dirisha hili linalenga hasa kwa waombaji wa mara ya kwanza wanaotoka katika ngazi ya kijamii

**2. DIRISHA LA KIWANGO CHA KATI**
Miradi iliyo chini ya Dirisha hili inapaswa kuzingatia mipango ya kusaidia mashirika ya haki za wanawake, wasichana na watoto ili kujenga/kuimarisha uwezo husika wa kidhana na shirika, na utaalamu wa kuunganisha na kubadilishana maarifa na harakati za wanawake na wasichana.
- Muda wa utekelezaji unapaswa kuwa kati ya miezi 6 na mwaka 1
- Lazima ilenge kutoa sauti kwa wanawake, wasichana, na watoto waliopembezoni kuhusu masuala yaliyotengwa kama ilivyoainishwa katika wito wa pendekezo.
- Dirisha liko wazi kwa shughuli zinazolenga wanawake na wasichana katika ngazi za mitaa na kitaifa, ambayo inahitaji fedha kwa ajili ya kuimarisha shirika ikiwa ni pamoja na mabadiliko au inajengea kwenye ya ruzuku ya awali ili kuimarisha ushirikiano wa kimkakati na mitandao katika harakati za wanawake katika ngazi tofauti.

**3. DIRISHA LA MIKAKATI**
Dirisha la Kimkakati linakusudiwa kufadhili miradi ya muda mrefu (hadi miaka 2) kwa shughuli zinazolenga juhudi za utetezi wa haki za wanawake/jukwaa/ujenzi wa Mtandao. Dirisha hilo pia linaweza kutumika kusaidia Asasi na Taasisi ambazo zinakua na ambazo zinahitaji usaidizi wa ufadhili ili kujenga uwezo wa kitaasisi na shirika hasa wapokeaji wa dirisha la kati wanaohitimu na kufanya kazi katika ngazi ya Kitaifa (Mashirika ya Kitaifa ya Haki za Wanawake, Mashirika ya Wanawake yenye uwezo wa kujenga harakati za Pamoja)

Ruzuku katika dirisha hili pia inaweza kusaidia kazi ya harakati mbalimbali za wanawake, wasichana na watoto. Mashirika ya Haki za Kifeminia yaliyo na uwezo husika wa kitaasisi na utaalam ikiwa ni pamoja na kuendesha mitandao na ujuzi wa kufanya kazi na washirika wengine (wa kijamii na kitaifa) ili kuimarisha mikakati ya kujenga harakati za pamoja za wanawake katika sekta zote zinahimizwa kutuma. Kwenye dirisha hili, tunapokea mapendekezo ya miradi ambayo yanalenga kuanzishwa au kuongeza kasi ya hatua ambazo zinakuza vitendo vya pamoja vya utetezi, majukwaa jumuishi, Mitandao ya kukuza ujuzi wa uandishi, mitandao na kujifunza katika sekta mbali mbali za wanawake, wasichana na watoto nchini.i.

**TUNATAFUTA NINI?**
Waombaji wanapaswa kujitahidi kulinganisha katika mapendekezo yao kanuni muhimu za muongozo zilizoainishwa hapa chini:

I. **KUOANA KWA MALENGO YA MRADI NA MAHITAJI MAKUU YA KIJINSIA KATIKA JAMII**
- Andiko ambalo linaonyesha jinsi malengo yatakavyokidhi matamanio ya wadau katika kuchangia juhudi za kuleta usawa wa kijinsia na ukombozi wa fikra katika maeneo yaliyoainishwa kutekelezwa na mradi

II. **UWEZO WA MTANDAO, SHIRIKA/KIKUNDI & UFAHAMU WA TATIZO LA MSINGI LA KUTATULIWA NA MRADI**
- Andiko la mradi linapaswa kuhakikisha uhusiano thabiti kati ya tatizo la kushughulikiwa na mikakati na matokeo yanayoweza kupimika yanayotarajiwa kupatikana kutokana na mradi
- Andiko la mradi linapaswa kuakisi ushiriki wa washikadau mbalimbali (ndani ya mtandao wa wanawake na katika mitandao mingine) katika utekelezaji wa kuunda/kuimarisha mitandao ya utendaji kazi, mitandao na majukwaa (hasa kwa madirisha 2&3)
- Andiko la mradi linapaswa kutumia miundo inayoonyesha uendelevu, uvumbuzi, ubunifu.
- Maandiko hayo ya mradi yanapaswa kujumuisha shughuli zitakapopangwa kufanyika katika siku za maadhimisho ya kikanda na kimataifa kama vile Siku ya Kimataifa ya Mtoto wa Afrika, Siku ya Kimataifa ya Wanawake wa Vijijini na Siku 16 za Uanaharakati.

**Mahitaji mahususi:**

**Maombi ya Ruzuku hizi yatafuata utaratibu huu:**
1. **Tembelea tovuti ya WFT Trust (www.wft.or.tz) ili kupakua fomu ya pendekezo**
2. **Jaza fomu ya pendekezo (isizidi kurasa 12) inayoelezea wazo au mpango uliopendekezwa.**
3. **Ambatanisha nakala ya usajili na katiba ya shirika kwenye pendekezo kisha utume kupitia barua pepe kwa grants@wftrust.or.tz**
**AU**
4. **Jaza maombi kisha uwasilishe ofisini au yatume kwa anuani ifuatayo:**

Mkurugenzi Mtendaji
Women Fund Tanzania Trust
S.L.P. 79235, Dar es Salaam.

216703102

**Kwa maelezo zaidi, tafadhali piga simu: +255 753 912 130**

**Tafadhali kumbuka:**
**Hakuna ofa, malipo, zawadi, uzingatiaji au manufaa ya aina yoyote, ambayo yanajumuisha au yanaweza kufasiliwa kuwa ni kitendo haramu au ulaghai, yatatolewa, moja kwa moja au isiyo ya moja kwa moja, kama kichocheo au zawadi kwa ajili ya mafanikio ya ombi.**

**Tarehe ya mwisho ya kuwasilisha itakuwa Jumatatu, Machi 7, 2022 saa Nane mchana.**
**Waombaji waliofanikiwa watajulishwa kabla ya tarehe 29 Aprili, 2022. Ikiwa hujajulishwa kufikia wakati huo, tambua kwamba ombi lako halijafanikiwa.**

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

## Kila la kheri Simba SC michuano ya kimataifa

**KESHO** ni siku nyingine bendera ya Tanzania itapeperushwa katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika ambayo yanaandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Tanzania imebakiza timu moja tu inayoshiriki katika mashindano hayo ambayo ni Simba baada ya Yanga, Azam FC, Biashara United zote za Bara kutolewa mapema katika michuano hiyo ya kimataifa.

Kwa upande wa Zanzibar, timu za KMKM na JKU pia zilitolewa mapema katika michuano hiyo na kuifanya Simba kuwa wawakilishi pekee wa Tanzania waliobakia kwenye mashindano hayo ya juu kwa Afrika kwenye ngazi ya klabu.

Simba iko katika Kundi D ikiwa pamoja na RS Berkane ya Morocco, ASEC Mimosas (Ivorry Coast) na USGN ya Niger.

Mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba walioko chini ya Kocha Mkuu Mhispania Pablo Franco walihamia katika michuano hiyo baada ya kutolewa na Jwaneng Galaxy ya Botswana kwenye mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Simba inaingia katika hatua hiyo ya makundi kwa kuwawakilisha Watanzania wote na kufanya kwao vizuri kutaendelea kuitangaza na kuipa heshima nchi yetu ambayo kwa miaka ya hivi karibuni imekuwa pia ikiiwakilisha vyema Afrika Mashariki.

Wadau na mashabiki wa soka huu ni wakati wa kuungana na kuiombea Simba mafanikio kwa sababu kusonga kwao mbele kwenye michuano hiyo kutasaidia kuipa nchi nafasi ya kupata tiketi nne katika msimu ujao wa mashindano hayo yanayoandaliwa na kusimamiwa na CAF. Tunaamini kama wadau watashirikiana kwa dhati kuhakikisha Simba inafanya vizuri kwenye mechi zake za nyumbani na ugenini kwenye hatua hii ya makundi, basi nafasi ya kusonga mbele itakuwa nyepesi na haitakuwa na mabonde kama ambavyo inatarajiwa.

Kimsingi kila mdau anafahamu kusonga mbele kwa Simba hakutaifaidisha klabu hiyo peke yake, bali matunda ya matokeo chanya yatakayovunwa kwenye hatua hiyo, yataletea nchi faraja ya kupata wawakilishi wengi zaidi katika msimu ujao wa michuano hiyo ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho Afrika.

Licha ya Simba kuwa na uongozi wake, naamini viongozi wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), wameshakutana na wawakilishi hao ili kuhakikisha kila jambo linalotakiwa kutekelezwa kuelekea hatua hiyo muhimu limekamilika kwa sababu ya kuweka mbele maslahi ya nchi na si kuonekana wanaipendelea.

Inajulikana wazi Simba ikiendelea kusonga mbele, itavuna fedha zaidi kutoka CAF, hali kadhalika TFF pia hupata fungu lake lakini wafanyabiashara mbalimbali kuanzia wa usafiri, hoteli na vyakula hupata fedha kutokana na uwapo wa michezo hiyo ya kimataifa.


Vitendo vya kuendelea kuwashangilia wageni tuone ni vya kishamba kwa sababu mbali ya kujiombea wenyewe dua mbaya, lakini vinaendelea kulidhalilisha taifa kwa sababu mashabiki wa nchi nyingine hawafanyi hivyo.

Pia tunawakumbusha wachezaji wa Simba kuhakikisha wanacheza kwa viwango vya juu ili kuhakikisha timu yao inafikia malengo iliyojiwekea ya kutinga hatua ya nusu fainali, lakini wafahamu hatua hii ni daraja lingine linaloweza kuwaweka sokoni na hatimaye kunununliwa na klabu za nje ya Tanzania au bara la Afrika.

Tunawashauri wachezaji watakaopata nafasi ya kucheza mechi za hatua hii ya makundi, wajue si wanafuatiliwa na makocha wa ndani, michuano hii hufuatiliwa na mawakala na makocha kutoka sehemu mbalimbali duniani ikiwa inafuata kwa ngazi ukiondoa Ligi ya Mabingwa Afrika na baada ya kumalizika kwa fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika.

Tuungane pamoja kuiombea dua njema Simba kwa faida ya Tanzania na kusahau upinzani wa hapa kwa faida ya kizazi kijacho ambacho kinajifunza kutokana na yale wanayoshuhudia sasa kutoka kwa wakubwa zao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

## Waamuzi wasipewe presha nje ya uwanja

Na Adam Fungamwango

**KATIKA** nchi za wenzetu kwa sasa mtu yeyote awe kocha, mchezaji au kiongozi atakayemsema mwamuzi vibaya basi atapigwa faini na kufungiwa mechi kadhaa.

Kwa sababu wanajua ukiruhusu watu kuanza kusakama waamuzi, basi kila mtu akikosa matokeo kibilio linaweza kuelekea kwa waamuzi.

Bahati nzuri kwa sasa baadhi ya wenzetu wameendelea kwa kuwa na VAR, ambayo ni mashine ya msaada kwa waamuzi. Hii imekuwa kama mwarobaini wa waamuzi wengi nchi nyingi barani Ulaya na sehemu nyingine za dunia.

Afrika bado ni sehemu chache sana ambazo zina VAR. Sehemu kubwa ya soka la Afrika bado linachezeshwa kizamani.

Hivi majuzi, Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli na Msemaji wa klabu hiyo, Haji Manara, waliitisha mkutano na Waandishi wa Habari, pamoja na mambo mengine walieleza kutoridhishwa na baadhi ya uamuzi wa waamuzi katika mechi zinazoihusisha timu yao.

Wakati wakidai wanachezeshwa vibaya, wakaenda mbali zaidi na kudai waamuzi hao wamekuwa wakiichezesha Simba kwa namna ya kuibeba.

Yaani Simba imekuwa ikinufaika na uamuzi mbovu wa waamuzi. Wakadai hawalalamiki, ila wanawakumbusha.

Kali kuliko zote, kesho yake wazee wa Yanga nao wakaibuka, nao wakaongea maneno yanayofanana na hayo hayo ya Manara na Bumbuli.

Ila wao wakaenda mbali zaidi na kudai kuna mkubwa mmoja serikalini amekuwa akilazimisha Shirikisho la Soka Nchini (TFF), kuwaambia waamuzi waibebe Simba.

Mkutano na maneno hayo ya wazee yanawafanya TFF nao kuibuka na kusema haichezeshi ligi kwa maelekezo ya mtu yoyote yule, bali inaendeshwa na Bodi ya Ligi chini ya Kamati ya Uendeshaji na Usimamizi wa Ligi.

Ilikuwa ni wiki ya mambo mengi sana, kwani Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, aliahidi kumtafutia fedha, Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mohamed Mchengerwa, kwenye bajeti ijayo kwa ajili ya kuweka mashine za VAR ili zitumike kwenye mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Na hiyo ni baada ya Yanga kutoa suluhu ya bila kufungana dhidi ya Mbeya City, akidai kama kungekuwa na VAR, basi Yanga ingeondoka na ushindi wa bao 1-0, kwani Fiston Mayele alikuwa kwenye nafasi ya kufunga bao na hakuwa ameotea kama mwamuzi namba moja alivyotafsiri.

Ukiangalia Ligi Kuu ya msimu huu sidhani kama kuna timu ambayo haijanufaika, au kuathirika na uamuzi mbaya, au makosa ya waamuzi.

Siwezi kuyaainisha hapa kwa sababu ni mengi sana. Nampongeza Nchemba kwa kutaka kuleta VAR. Lakini swali linakuja, kwa nini amesema hayo wakati tukio limeihusu Yanga?

Halikuwa tukio la kwanza, lakini ameonekana kuja na mpango mkakati huo baada ya Yanga kunyimwa nafasi ya bao.

Hata hivyo bado nimpongeze kwa hilo, lakini pia hata viwanja navyo virekebishwe ndivyo VAR ije kama alivyosema mwenyewe.

Ila nimkumbushe tu, klabu za Simba na Yanga ndizo zinazoongoza kwa kubebwa na makosa ya kibinadamu ya waamuzi. Nadhani hata kimoyomoyo baadhi ya viongozi wa timu hizo watakuwa hawaitaki kabisa.

Najua kuwa VAR ikija, zitakazoathirika zaidi ni klabu hizo na zitaanza kutafuta sababu nyingine ili ziondolewe au kutiwa kasoro kwa sababu tu kila kitu kitakuwa kiko sawa.

Tukirudi kwa waamuzi, nadhani wasipewe presha sana. Kinachoonekana sasa ni kuna makusudi fulani ya kuwafanya wasitoe penalti kwa timu ambayo inapaswa kupata, na watoe pale ambapo haipaswi, ili mradi tu wasilaumiwe.

Na hata zinapotakiwa kuongezwa dakika nyingi kwa upotevu wa dakika zisiongozwe, huu sasa utakuwa si mpira.

Viongozi wasiwatie presha waamuzi wetu, badala yake wawaache wachezeshe hadi hapo VAR zitakapokuja.

Kama hata hao wa nje, wanafanya makosa na kusaidiwa na VAR, iweje leo hawa wa bongo wanaofanya makosa na hakuna VAR walaumiwe na kulalamikiwa kama wameua mtoto wa jirani?

Kabla Nchemba kushauri na kusaidia kuja kwa VAR nchini, niliwahi kushauri TFF kuleta waamuzi kutoka nje ya nchi kuchezesha baadhi ya mechi, lakini halikufanyiwa kazi.

Nadhani imefika wakati wa VAR na pia baadhi ya waamuzi kutoka nje kusaidia mechi kwenye kuamua kwa sababu wao wakikosea itaonekana ni makosa ya kibinadamu na hawapendelei. Hata hivyo kwa sasa tusiwatie waamuzi wetu presha kwa makosa ya kawaida kabisa.

## Mbaroni kwa tuhuma za kuingia nchini kinyemela

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WATU 15 wamekamatwa na Idara ya Uhamiaji wilayani Kahama mkoani Shinyanga wakituhumiwa kuwa ni wahamiaji haramu kutoka Burundi.

Watuhumiwa hao wanadaiwa kuingia nchini bila kuwa na vibali maalumu na kuanza kujihusisha na shughuli za ujasiriamali kinyume cha sheria.

Vilevile, Mtanzania mmoja amekamatwa katika msako huo uliofanywa wilayani Kahama.

Ofisa Uhamiaji Wilayani Kahama, Salumu Rashindi, alibainisha hayo jana alipozungumza na vyombo vya habari ofisini kwake, akisema kila mwezi wamekuwa wakikamata zaidi ya wahamaiji haramu 50 na kuwafikisha mahakamani na wengine kuwarejesha kwenye nchi wanazotoka.

Alisema asilimia 80 ya wajasiriamali wadogo walioko mjini humo ni wahamiaji haramu na wengi wao ni raia wa Burundi na wamekuwa wakitumiwa na wenyeji kwenye shughuli hizo kwa sababu wanawalipa ujira mdogo kulinganisha na Watanzania.

Rashidi aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni pamoja na: Ndaisenga Chilibeli (20); Niyonhuru Pole (31); Richard Alumukiza (18); Ndikumana Nyandu (19); Nakanutimana Jonas (19); Ikulubana Joshua (17); Wizimana Gerald (21); Habimana Ejide(20); na Ikundilo Godefrua (16).

Wengine ni: Joseph Philipo (38); Nduwayo Elize (16); Justini Crode (20); Wizimana Nicolaus (23); Kulwa Elias (18); Ndaikyekukia Erick (17); na na Mtanzania Derefa Michael (48) ambaye ni meneja wa baa ya Twiga iliyoko Kata ya Mhongolo, Manispaa ya Kahama, akituhumiwa kuwapa hifadhi watu hao.

Alisema wanapoingia nchini wanaajiriwa kama walinzi kwenye nyumba za kulala wageni, kuuza chips, kuchoma nyama, kuuza karanga mitaani, kuuza miwa na kwa sasa wanazungumza Kiswahili kama Watanzania.

"Kila mwezi tumekuwa tukikamata wahamiaji haramu zaidi ya 50 na kuwafikisha mahakamani na baadhi yao kuwarejesha nchini mwao, lakini bado wanarejea na tunawataka kuwafikisha mahakamani adhabu zake zinakuwa kali zaidi," alisema.

"Sheria ya Uhamiaji Sura ya 54 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2016 inasema kwa raia wa Tanzania atakayebainika kusafirisha raia wa kigeni atatozwa faini ya Sh. milioni 20 au kwenda jela miaka 20 na chombo au nyumba iliyotumika kumhifadhi vitataifishwa," alionya.

Mmoja wa watuhumiwa hao, Kulwa Elias, alidai anatoka Changuzo, Burundi na aliingia nchini kwa ajili ya kutafuta maisha.

Alisema nchini mwake hali ya maisha ni ngumu na aliingia Tanzania kwa kupitia Wilaya ya Kakonko mkoani Kigoma akiwa na kibali ambacho kimeisha muda wake Februari 6 mwaka huu.

# Jaji Mkuu awabana majaji utoaji wa haki

**Na Mary Gwera,** ARUSHA

JAJI Mkuu wa Tanzania, amewataka majaji wafawidhi wa Mahakama Kuu kudhibiti ucheleweshaji wa mashauri mahakamani ili kuhakikisha haki inapatikana kwa wakati.

Prof. Ibrahim Juma alitoa agizo hilo juzi wakati wa ufunguzi wa kikao kazi cha majaji wafawidhi jijini Arusha, akisisitiza kuwa kwa kufanya hivyo, watakuwa wamechangia utekelezaji wa dhima ya Mahakama ya Tanzania ya Upatikanaji wa Haki kwa Wote na kwa Wakati. "Ninyi ni viongozi na pia ni watu muhimu sana katika utekelezaji wa sheria, hivyo mnatakiwa kuwa mstari wa mbele kusimamia suala la uondoshaji wa mashauri kwa wakati pamoja na kufanya uboreshaji wa huduma za mahakama kwa ujumla," aliagiza.

Prof. Juma aliainisha baadhi ya mashauri yanayolalamikiwa kucheleweshwa kuwa ni ya mirathi na jinai huku akiwasisitiza majaji kufanya jitihada binafsi katika kanda wanazosimamia ili kuwezesha kumaliza mashauri kwa wakati.

"Ni muhimu kuzingatia mikakati ya taasisi kuhusu uondoshaji wa mashauri, mbali na mikakati hii ni rai yangu kwenu majaji wafawidhi kuwa na mikakati binafsi ya kikanda ambayo inalenga kuboresha zaidi utoaji wa haki kwa wakati," alisisitiza.

Aliongeza kuwa jaji mfawidhi ni msimamizi mkuu katika kanda au divisheni, hivyo panapotokea mabadiliko ya sheria au kanuni zinazogusa shughuli za utoaji haki, ni wajibu wake kuyaelewa mabadiliko hayo mapema na kuwaelimisha watumishi wote kuhusu mabadiliko hayo.

"Huwezi kufanikiwa katika nafasi yako ya Jaji Mfawidhi endapo huielewi Tanzania na mazingira mbalimbali yanayoizunguka Tanzania.

"Hivyo hivyo, huwezi kufanikiwa endapo huwaelewi watumishi wa kada mbalimbali wa mahakama. Jaji mfawidhi hawezi kufanikiwa endapo hawaelewi wadau na watumiaji wa mahakama," alionya.

Mbali na suala la udhibiti wa ucheleweshaji wa mashauri, Prof. Juma aliwakumbusha majaji wafawidhi kutosahau kutekeleza kaulimbiu ya Wiki ya Sheria ya Mwaka huu inayosema 'Zama za Mapinduzi ya Nne ya Viwanda: Safari ya Maboresho Kuelekea Mahakama Mtandao'.

Madhumuni ya kikao kazi hicho cha siku mbili ni pamoja na kujenga ufahamu wa pamoja kuhusu hatua muhimu za kufuatwa hadi Mahakama-Mtandao, kujadili namna bora ya kukabiliana na wasiwasi, mitazamo na tamaduni hasi zilizojificha miongoni mwa watumishi dhidi ya matumizi ya teknolojia katika ufanisi na uwazi wa utoaji haki.



Ofisa Uhamiaji wa Wilaya ya Kahama, mkoani Shinyanga, Salum Rashidi (kulia), akionyesha kwa waandishi wa habari jana, wahamiaji haramu 15 raia wa nchi ya Burundi, waliokamatwa kwa kosa la kuingia nchini bila kibali na kujishughulisha na kazi mbalimbali ikiwemo ujasiriamali. **PICHA: SHABAN NJIA**

## Washikiliwa polisi kwa tuhuma meno ya tembo

**Na Neema Hussein,** KATAVI

JESHI la Polisi Mkoa wa Katavi linawashikilia watu wawili kwa tuhuma za kukutwa na meno mawili ya tembo.

Watuhumiwa hao wanadaiwa walikamatwa na polisi wakati wakiyasafirisha meno hayo kwa kutumia pikipiki yenye namba za usajili MC 410 BQW aina ya SanLG huku wakiwa wameyaweka kwenye mfuko wa sandarusi. Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Katavi, Ali Makame, aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Beno Martias (68) na Nova Issaka (45).

Kamanda Makame alidai watuhumiwa walitenda kosa hilo Februari 10 mwaka huu katika Kijiji cha Inteka A Wilaya ya Mpanda mkoani Katavi.

Alisema upelelezi wa tukio hilo bado unaendelea na mara baada ya kukamilika, watuhumiwa watafikishwa mahakamani kujibu tuhuma zinazowakabili.

Mbali na tukio hilo, jeshi hilo pia limekamata silaha moja aina ya gobole na nyama ya nyati kilo 60.

Makame alisema kuwa Februari 7, mwaka huu, katika Kijiji cha Masigo, mtu mmoja ambaye jina lake bado halijafahamika, aliyekuwa akiendesha baiskeli huku amebeba mzigo, baada ya kugundua anafuatiliwa na polisi aliteleketeza baiskeli hiyo na kukimbia.

Alisema mtu huyo alitokomea porini na baada ya kufanya upekuzi kwenye mzigo huo, kulikutwa silaha hiyo na nyama ya nyati.

Kamanda Makame alisema msako mkali wa kumtafuta mtuhumiwa unaendelea kwa kushirikiana na uongozi wa Kijiji cha Masigo.



Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Benki ya Mwanga Hakika, Muhandisi Ridhuan Mringo (kulia), akikabidhi msaada wa meza na viti 474 vyenye thamani ya Sh. milioni 30 kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mwanga, Mwajuma Nasombe, kwa ajili ya Shule za Sekondari wilayani humo. Anayeshuhudia mwenye kaunda suti ya buluu ni Mkuu wa Wilaya hiyo, Abdallah Mwaipaya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mahakama Kuu yabariki uongozi wa Lipumba CUF

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dar es Salaam imekataa kutoa amri ya kumvua uongozi Mwenyekiti wa Chama cha Wananchi (CUF), Prof. Ibrahim Lipumba, baada ya kutupilia mbali maombi ya kutaka avuliwe uongozi.

Uamuzi huo dhidi ya Prof. Lipumba, Katibu Mkuu wa CUF, Arubu Shamis na Naibu wake, Magdalena Sakaya na Bodi ya Wadhamini ya CUF, ulitolewa jana mbele ya Jaji Ephery Kisanya.

Maombi hayo yaliwasilishwa mahakamani huko na Makamu Mwenyekiti wa CUF, Zanzibar Mussa Haji Kombo na Juma Maimbo ambaye ni mwanachama wa chama hicho.

Akisoma uamuzi huo, Jaji Kisanya alisema mahakama imetupilia mbali maombi hayo kwa kuwa waleta maombi wameshindwa kutimiza vigezo viwili kati ya vitatu muhimu vitakavyosababisha mahakama ikubaliane na maombi yao.

"Waleta maombi wameshindwa kuithibitishia mahakama hasara ambayo inaweza kupatikana kama maombi yao hayatakubaliwa kwani hawakuweza kuwasilisha mahakamani ushahidi juu ya hasara hiyo.

"Waleta maombi katika kiapo chao walidai Msajili wa Vyama vya Siasa anaweza kufuta usajili wa chama hicho lakini hata hivyo hawajawasilisha mahakamani barua ya msajili huyo akionyesha nia yake ya kutaka kufuta usajili wa CUF.

"Wadai hawajaeleza kuwa kuondolewa kwa nafasi za uongozi za wadaiwa kutakavyoweza kuzuia kufutwa kwa chama hicho," alisema.

Jaji Kisanya alisema kigezo cha pili ambacho hawakukidhi ni mizania kwamba ni kwa namna gani waleta maombi watapata hasara kubwa kuliko wajibu maombi, hivyo maombi yalitupwa.

Wakati wa usikilizwaji wa maombi hayo, Wakili Hashim Mziray alidai wamewasilisha maombi hayo kutokana na uvunjifu wa katiba ya chama hicho ya mwaka 1992 toleo la mwaka 2014 ambalo limevunjwa na toleo la mwaka 2019 uliofanywa na wadaiwa hao ambao ni viongozi wa CUF.

Alidai mabadiliko yaliyofanywa na wadaiwa yameenda kinyume cha kilichoamuliwa na Mkutano Mkuu wa CUF wa mwaka 2019 kwa kuwa kuna baadhi ya vifungu havikupaswa kurekebishwa.

Alidai katika Katiba hiyo kuna kitu kimeongezwa ambacho hakikujadiliwa na Mkutano Mkuu ambacho ni 'Kamati ya Itifaki na Udhibiti', hayo yalifanywa na wadaiwa na katika majibu ya kiapo chao hawakuambatanisha Katiba ya CUF, hivyo chama kipo katika hatari ya kupoteza usajili wake'.

## Msako wanafunzi watoro warindima

**Na Richard Makore,** MWANZA

UONGOZI wa Mkoa wa Mwanza umefanikiwa kuwarejesha shuleni wanafunzi 121 walioacha masomo kutokana na sababu mbalimbali zikiwamo za utoro na ujauzito kupitia mpango maalumu wa kuwasaka vijijini na mitaani ili kuwarejesha shuleni kuendelea na masomo.

Maofisa elimu wa kata wamepewa kazi hiyo ya kuwasaka wanafunzi hao kupitia wenyeviti wa mitaa na vijiji ili kuhakikisha wanarejea shuleni.

Wanafunzi 181 waliomaliza darasa la saba mwaka jana na kushindwa mitihani yao, pia wamerudishwa shule kwa ajili ya maandalizi ya kurudia mitihani ili waweze kujiunga na kidato cha kwanza.

Akizungumza na Nipashe jana ofisini kwake jijini Mwanza, Ofisa Elimu mkoani Mwanza, Martin Nkwabi, alisema msako huo unaendelea hadi Machi 30 mwaka huu.

Alisema wanafunzi hao wanatakiwa kurejea shuleni kwa hiari na maofisa elimu wametakiwa kutembelea shule za sekondari ili kujua idadi ya wanafunzi walioacha masomo.

Akizungumzia takwimu za wanafunzi waliorejeshwa shuleni kuanzia Januari, mwaka huu, Nkwabi alisema wanafunzi 81 tayari wamerejea shule kupitia mfumo usiokuwa rasmi.

Alisema wanafunzi 40 walioacha shule kutokana na sababu mbalimbali, wamerejeshwa shuleni kupitia mfumo rasmi.

Alisema kati ya wanafunzi hao, 14 waliacha masomo kutokana na kupata ujauzito na 26 waliacha kwa kufukuzwa kwa utoro.

Akizungumza takwimu za mwaka 2020, Nkwabi alisema wanafunzi 61 waliacha shule kutokana na ujauzito na mwaka 2021 walikuwa 28.

Alisema tangu msako huo kuanza, wameendelea kupokea wanafunzi na kwamba ana imani ifikapo Machi 30, idadi hiyo ya wanafunzi kurejea shule itaongezeka.


## NOTISI / TANGAZO

**MUDU COMPANY LTD, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD,LEGENDS AUCTION MART LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,CHAMPION AUCTION MART,MAKI RECOVERIES LTD,PSALM AUCTION MART,MALAPA AUCTION MART,HEDANE ENTERPRISES LTD,KILICRAALS AUCTIONEER, DESTENI COMPANY LIMITED, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS,JY AUCTIONEERS CO.LTD, SMARKCORE GROUP LTD, WAUNGWANA AUCTION MART LTD, BEST GROUP LTD, NGOMENI AUCTION MART,MOPEH COMPANY LTD,KOTI BROTHERS LTD,MBUZAX AUCTION MART kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muunganowa Tanzania, chini ya benki ya AKIBA COMMERCIAL BANK PLC, tunatoa notisi ya kulipa madeni kwa wadaiwa wafuatao ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.**

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| KARIAKOO | UPENDO GODFREY NYANGE | NYUMBA | GODFREY ERASTO NYANGE | BONYOKWA | 04/03/2022 SAA 3:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KARIAKOO | RAMADHANI KITWANA IBRAHIM | NYUMBA | MARIAM KITWANA IBRAHIM | TABATA LIWITI | 04/03/2022 SAA 06:00 MCHANA NA KUENDELEA |
| KARIAKOO | ATHUMANI ABDUL MAKWARUZI | NYUMBA | ATHUMANI ABDUL MAKWARUZI | KINYEREZI | 04/03/2022 SAA 09:00 MCHANA NAKUENDELEA |
| KARIAKOO | FARIDA AYUBU MILLANGA | NYUMBA | FARIDA AYUBU MILLANGA | CHANIKA | 08/03/2022 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KARIAKOO | JUTIA ABDALLAH SANZE | NYUMBA | JUTIA ABDALLAH SANZE | PUGU | 08/03/2022 SAA 8:00 MCHANA NAKUENDELEA |
| KARIAKOO | ABDALLAH SAIDI CHIPALA | NYUMBA | ABDALLAH SAIDI CHIPALA | KISEMVULE | 28/02/2022 SAA 3:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | HAJI HARAMBE BIBOZE | NYUMBA | HAJI HARAMBE BIBOZE | VIKINDU MASHARIKI | 28/02/2022 SAA 6:00 MCHANA NAKUENDELEA |
| ILALA | SWALIHINA JUMA KALYANGO | KIWANJA | SWALIHINA JUMA KALYANGO | KIVULE | 09/03/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| TEMEKE | BETTY BENSON KAGARUKI | NYUMBA | BETTY BENSON KAGARUKI | MBEZI MSAKUZI | 10/03/2022 SAA 04:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| ARUSHA | BARAKAELI KUNDANDUNI MBISE | NYUMBA | BARAKAELI KUNDANDUNI MBISE | KINGORI-ARUMERU | 02/03/2022 SAA 4;30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | VALENCE WILLIAM GALINOMA | NYUMBA | VALENCE WILLIAM GALINOMA | MOSHONO | 28/02/2022 SAA 7:00 MCHANA NA KUENDELEA |
| ARUSHA | ISACK BALTAZAR MMASY | KIWANJA | ISACK BALTAZAR MMASY | TERRAT ARUSHA | 04/03/2022 SAA 04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | MASANJA JAMES WANNA | KIWANJA | MASANJA JAMES WANNA | TERRAT ARUSHA | 08/03/2022 SAA 04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MOSHI | PATRICK APOLINARI MTEI | NYUMBA | PATRICK APOLINARI MTEI | BOMANG'OMBE | 28/02/2022 SAA 7:00 MCHANA NA KUENDELEA |
| MOSHI | JULIUS STANLEY MALYA | NYUMBA | JULIUS STANLEY MALYA | BOMANG'OMBE | 28/02//2022 SAA 7:00 MCHANA NA KUENDELEA |
| MOSHI | ALLEN BARAKAEL MMARI | NYUMBA | ALLEN BARAKAEL MMARI | SANYA JUU | 03/03/2022 SAA 04:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba au Kiwanja ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2. Ikiwamnunuziatashindwakutimizashartilolote la mnada kuhusiana na malipo yaawali,hatarudishiwapesayoyotealiyokwishailipa.
3. Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.**0765999000/0754376493/0715467455**
4. Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi benki bila gharama yeyote.

216702902



# Mbunge alia uhaba wa watumishi afya, elimu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Nanyamba (CCM), Abdallah Chikota, amesema sekta za elimu na afya zinakabiliwa na uhaba mkubwa wa watumishi huku akiiomba serikali kutoa kibali maalumu cha ajira ili kukabiliana na hali hiyo.

Chikota aliyasema hayo juzi bungeni alipokuwa akichangia taarifa ya Kamati ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii.

Alisema kutokana na hali ilivyo kwenye halmashauri baada ya kujengwa miundombinu ya madarasa na vituo vya afya, ni vyema serikali ikachukua hatua za makusudi kuajiri watumishi wa sekta hizo.

"Kazi kubwa ambayo imefanywa na Rais Samia Suluhu Hassan ya ujenzi wa madarasa 15,000, vituo vya afya, faida za ujenzi wa miundombinu, haitaonekana kama upungufu huu utaendelea. Naomba serikali ichukue hatua za makusudi kutoa kibali maalumu kuajiri walimu na watumishi wa sekta ya afya."

"Naiomba serikali yangu sikivu itoe kibali maalumu kama ilivyofanya miaka ya nyuma tulivyokuwa na uhaba wa wahasibu," alisema.

Kuhusu Chuo cha Ualimu Mtwara, Chikota alisema kulikuwa na mapendekezo vyuo vitatu, kikiwamo Mtwara , viwe vyuo vikuu vishiriki ili kuongeza idadi ya walimu wa sayansi na kutaka serikali itekeleze azma hiyo.

"Chuo cha Ualimu Dar es Salaam na Mkwawa tayari vimekuwa vyuo vikuu vishiriki bado Mtwara. Naomba serikali itekeleze azma yake kwa kuwa Mtwara kuna miundombinu yote muhimu inayohitajika. Tukiwa na Chuo Kikuu Kishiriki Mtwara, wana Mtwara wengi watahamasika kusoma kwa kuwa chuo kitakuwa jirani kwao," alisema.

Hata hivyo, alisema kuna muingiliano wa majukumu kati ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na wizara za kisekta za elimu na afya.

"Juzi tulifanya kikao cha kuwakutanisha TAMISEMI na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kwenye utekelezaji kuna mwingiliano na hii iko wazi tu. Ile D by D, ugatuaji bado haujaeleweka vizuri. Kuna watumishi bado hawajaelewa dhana ya ugatuaji na hata viongozi," alisema.

Alisema tatizo lililopo hakuna sheria ya ugatuaji isipokuwa ipo sera ya mwaka 1998 na kwamba ni wakati wa serikali kutunga sheria ya kusimamia ugatuaji ili kuondoa mwingiliano na kurahisisha utekelezaji wa majukumu.



Mbunge wa Viti Maalum kutoka Zanzibar, Asia Mwadini Muhammed, akichangia ripoti ya Kamati ya Ardhi na Maliasili, Bungeni jijini Dodoma juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mpango kuzindua sera ya mazingira

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, leo anatarajiwa kuzindua Sera Mpya ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021 ambayo imezingatia masuala mbalimbali ikiwamo mabadiliko ya tabia nchi.

Akizungumza jana katika upandaji miti eneo la Tambukareli jijini hapa ikiwa ni sehemu ya wiki ya uzinduzi wa sera hiyo, Katibu Mkuu wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mary Maganga, alisema katika wiki hiyo wananchi wamehamasika na kujitokeza kufanya shughuli mbalimbali zilizopangwa ikiwamo kupanda miti na kufanya usafi.

"Kila tulipokwenda kwa ajili ya kupanda miti tunakuta umati mkubwa wa watu. Mwamko ni mkubwa, tumefanya matukio haya si kwa Dodoma peke yake tunatarajia kuwe na mwamko mkubwa Watanzania wahamasike na kesho (leo) ndiyo kilele cha shughuli hii yote tunahitimisha kwa kuzindua sera mpya ya mazingira,"alisema.

Awali, Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi Wakala wa Huduma za Misitu (TFS) Kanda ya Kati, Mathew Kiondo, alisisitiza miti hiyo kutunzwa baada ya msimu wa mvua kuisha na kudhibiti mifugo.

"Si vizuri tukapanda miti leo halafu mwakani tena tunapanda sehemu hii hii tutakuwa tunapoteza nguvu na fedha za serikali kwa hiyo tuhakikishe tumepanda leo, tuite mkutano kama huu kuja kumwagilia maji kwa kuwa Dodoma kipindi cha ukame ni kirefu,"alisema.

Alibainisha kuwa TFS imejipanga kutoa miche kwa taasisi na kwa mtu mmoja mmoja na ipo ya kutosha na wapo tayari kutoa utaalamu wao.

Naye Balozi wa Mazingira na Mbunge wa Pandani, Mariam Omary Saidi, alihamasisha wakazi wa Dodoma kuhakikisha wanaitunza miti na mazingira ili kuifanya Dodoma kuwa ya kijani.

## Waunga mkono ujenzi wa soko, stendi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAFANYABIASHARA wa Soko la Sabasaba jijini Dodoma wameunga mkono mpango wa serikali wa kuwajengea soko na stendi mpya itakayokuwa na miundombinu ya kisasa ili kukidhi mahitaji ya sasa.

Wafanyabiashara hao waliyasema hayo jana kwenye mkutano wao na Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Steven Massawe, alisema wako tayari kupisha eneo hilo ambalo serikali inataka kuwekeza mradi wa ujenzi huo ili ufanyike kwa ufanisi.

Alisema hawapingi maendeleo ya serikali kwenye ujenzi wa soko na stendi bali kinachotakiwa kwa serikali ni kuhakikisha kunakuwepo ushirikiano kati yao na halmashauri ya jiji ili haki itendeke na kusiibuke migogoro.

Massawe alisema wana matumaini makubwa kuwa watafanya biashara zao kwenye miundombinu ya kisasa na hata thamani itaboreshwa, hivyo kinachotakiwa ni kuandaliwa mpango utakaowawezesha kufanya biashara kwenye maeneo yaliyo rafiki kwao na wateja.

"Wafanyabishara walio wengi ndani ya soko na watumiaji wa stendi hii ya Sabasaba wana mikopo, hivyo tunaiomba serikali kuhakikisha wanawaweka maeneo yatakayokuwa rafiki kwa biashara zao ili kurejesha fedha zao kwa wakati walizokopa kwenye taasisi mbalimbali za kifedha," alisema Massawe.

Mfanyabiashara mwingine, Julius Lugusi, aliiomba serikali mpango huo wa ujenzi wa soko na stendi kufanywa kwa uwazi kwa kukaa pamoja pande zote ili kusiwe na sintofahamu kwao na wengine wakajikuta wakikosa nafasi zao za kufanyia biashara.

Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri, aliwahakikishia wafanyabiashara hao kuwa serikali itatoa maeneo yatakayokuwa rafiki kwenye bidhaa zao pamoja na wateja wao kwa kipindi chote ambacho ujenzi utakuwa ukiendelea.

Shekimweri alisema kinachofanyika kwa sasa ni usanifu wa eneo hilo la soko la Sabasaba, kwa hivyo wafanyabiashara hao wanatakiwa kujipanga ili kupisha eneo lao na ujenzi utakapoanza kuwe huru kwa watakaojenga mradi huo.

"Kwanza naomba kuwashukuru wafanyabiashara wa soko hili la Sabasaba kwa kulikubali hitaji hilo la serikali la kujenga soko na stendi kwa ajili ya kulifanya kuwa la kisasa, hivyo niwahakikishie serikali itakuwa bega kwa bega kwa kipindi chote cha utekelezaji," alisema.

Pia aliutaka uongozi wa umoja wa soko hilo kuzingatia katiba yao katika kuhakikisha wafanyabiashara wote wanapata haki sawa wakati wa zoezi hilo utakapowadia bila ubaguzi kwa kuwa utakapokamilika utawanufaisha watanzania wote.

Aliwataka kuhakikisha haki za wafanyabiashara hazipotei kila mmoja anapatiwa na serikali itakuwa macho kuona watu wote wanaojishughulisha na biashara hawakosi nafasi zao kwa wale waliomo ndani ya soko hilo.





# Wizara yasema sheria za habari na usajili magazeti zimepitwa na wakati

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

NAIBU Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Khamis Abdallah, amesema Zanzibar inaongozwa na Sheria ya Habari na Sheria ya Magazeti ya mwaka 1988 ambayo imepitwa na wakati.

Amesema baadhi ya vipengele vyake havitekelezeki, hivyo kuna haja ya kuwapo kwa mabadiliko ya sheria hiyo.

Khamis aliyasema hayo jana katika kikao cha pamoja cha uwasilishaji wa maoni ya mswada wa Sheria ya Huduma za Habari kati ya Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi na wadau wa habari. Kikao hicho kiliandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Ofisi ya Zanzibar kupitia mradi wa boresha habari unaofadhiliwa na Internews.

Alisema hivi sasa serikali iko katika mchakato wa kuhakikisha kuwa na Sheria ya Habari ya kisasa inayotumika na kukidhi mahitaji ya sasa.

"Wizara tumepokea nyaraka mbili muhimu sana. Tumepokea rasimu ya Sera ya Habari na rasimu ya Sheria ya Habari na kwa sasa tunazifanyia kazi ili kuwa na sheria nzuri ya habari," alisema.

Khamis alisema wanataka kuona sekta ya habari inakuwa na viwango vya hali ya juu, weledi, uwezo na uhuru wa habari unapatikana na kukidhi viwango vya kikanda na kimataifa.

"Tutajitahidi sheria hii iwe imekidhi viwango vya kikanda na kimataifa ili waandishi wa habari wasikwazwe katika kufanya majukumu yao lakini pia wananchi wafaidike na huduma zinazotolewa na waandishi wa habari," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi, Mohamed Ahmada, alisema ili vyombo vya habari vifanikishe utekelezaji wa majukumu yake kwa jamii, ni muhimu kuwapo kwa sheria zinazo kwenda na mabadiliko ya wakati.

"Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi tunakubaliana na maoni ya kamati ya wadau kuhusu mapendekezo ya sheria ya habari ambayo lengo lake kubwa ni kuiwezesha jamii kupata taarifa za serikali bila vikwazo," alisema.

Mjumbe wa Kamati hiyo, Shaaban Ali Othman, alisema lazima wadau washirikishwe katika mapendekezo ya sheria ya habari kwa lengo la kuleta ufanisi na kuwa na sheria inayotekelezeka na kuondosha malalamiko.

Akiwasilisha maoni ya mapendekezo ya sheria ya huduma za habari, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Waandishi wa Habari za Maendeleo Zanzibar (WAHAMAZA), Hawra Shamte, alisema sheria hiyo inasisitiza umuhimu wa kupata habari kwa waandishi wa habari na vyanzo vyake ikiwamo serikali na kuondosha urasimu ambao ni kikwazo kikubwa.

Pia alisema Sheria ya Usajili wa Magazeti, wakala wa habari na vitabu ya mwaka 1988 imepitwa na wakati na haikidhi mahitaji ya wadau wa sekta hiyo katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.

"Urasimu ni miongoni mwa vikwazo kwa waandishi wa habari katika kupata habari. Katika sheria mpya inayopendekezwa, tunataka viondoshwe," alisema.

Ofisa Mwandamizi wa Baraza la Habari Tanzania (MCT) Ofisi ya Zanzibar, Shifaa Said Hassan, alisema mapendekezo yote yaliyofanywa katika sheria mpya ya huduma za habari ya mwaka 2021 lengo lake kubwa ni kuitambua na kuifanya kazi ya uandishi wa habari kuwa taaluma na kuepuka ubabaishaji mkubwa unaofanywa na watu wanaojipenyeza na kusababisha upotoshaji.



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari Zanzibar, Khamis Abdallah akijadiliana jambo na Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, baada ya kikao cha kujadili sheria ya habari, mjini Zanzibar juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Taasisi za maafa zaombwa ushirikiano

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NAIBU Mkurugenzi Mtendaji wa Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa, Muhsin Ali Muhsin, amewataka watendaji wa taasisi zilizomo katika utekelezaji wa mpango wa kukabiliana na maafa kufanya kazi kwa ushirikiano kwa mujibu wa mwongozo.

Muhsin aliyasema hayo jana katika ofisi za kamisheni hiyo, Maruhubi, wakati wa kujadili mwongozo wa kituo cha operesheni ya dharura na mawasiliano kwa wadau wa maafa.

Alisema masahihisho ya mwongozo huo yatasaidia utekelezaji bora wa majukumu ya kazi wakati maafa yakitokea.

Akiwasilisha mwongozo huo, Dk Fredrick Salukele kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, alisema muundo umehusisha wadau wote wa maafa pamoja na majukumu yao ya kiutendaji .

Alisema hatua zinahitajika kuchukuliwa iwapo dharura itatokea kwa kila mdau kutekeleza majukumu ambayo anapaswa kutekeleza kwa mujibu wa mwongozo.

Mwongozo wa kituo cha operesheni ya dharura na mawasiliano ni mwendelezo wa majadiliano na mapendekezo mbalimbali yanayotakiwa kubadilishwa kwa mujibu wa makubaliano ya wadau kwa pamoja waliomo katika mpango huo.

**Mwongozo wa kituo cha operesheni ya dharura na mawasiliano ni mwendelezo wa majadiliano na mapendekezo mbalimbali yanayotakiwa kubadilishwa kwa mujibu wa makubaliano ya wadau kwa pamoja waliomo katika mpango huo.**

# Bodi yapongezwa udhibiti wa vileo

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

WAJUMBE wa Baraza la Wawakilishi (BLW) wamepongeza Bodi ya Udhibiti wa Vileo kwa kuteua kampuni tatu kuingiza vileo kati tisa zilizojitokeza katika zabuni ya mwaka 2022.

Wakizungumza jana na waandishi wa habari katika ukumbi wa Baraza la Wawakilishi, Chukwani mjini Zanzibar, walisema tangu baraza kupitisha Sheria ya Vileo Na. 9 ya mwaka 2020, Bodi ya Udhibiti wa Vileo ilikuwa inavunja sheria kwa kutoa vibali kwa zaidi ya kampuni tatu.

Mwakilishi wa Shaurimoyo na waziri wa zamani wa SMZ, Hamza Hassan Juma, alisema kifungu cha 33(1) cha Sheria ya Udhibiti wa Vileo kimeweka sharti kampuni za uingizaji vileo mwisho tatu lakini mwaka 2021 kampuni nane zilipewa vibali kinyume cha sheria.

"Kwa kweli tunapongeza bodi mpya ya udhibiti vileo iliyoundwa na Rais wa Zanzibar. Kwa kweli wameanza vizuri, wanasimamia sheria kwa vitendo kama ilivyopitishwa na Baraza la Wawakilishi Zanzibar," alisema. Hata hivyo, alisema Bodi inapaswa kufanya uhakiki wa baa baada ya kuwapo malalamiko kutoka kwa wananchi kuwa baadhi ya baa zimefunguliwa karibu na makazi ya watu na maeneo ya huduma za jamii na kuwa kero kwa wananchi.

Alisema viongozi wa serikali za mitaa (masheha) pia wamekuwa wakisababisha matatizo kutokana na kutoa ruhusa za kuanzishwa baa katika makazi ya watu bila kuwashirikisha wananchi na kusababisha malalamiko baada ya baa kuanza kufanya kazi.

"Kuna baa zinahitaji kupigwa makufuli kwa sasabu zimekuwa kero kwa wananchi na maeneo ya huduma za jamii na makazi kama shule, nyumba za ibada na hospitali," alisema.

Mwakilishi wa Amani, Rukia Ramadhan Mapuri, alisema kwa mujibu wa Sheria ya Vileo kifungu cha 28(k), baa zinatakiwa kuwa umbali wa mita 1,000 kabla ya wahusika kupewa leseni na bodi ya vileo.

"Sheria ya Udhibiti wa Vileo kama itasimamiwa vizuri, itasadia kuondoa baa korofi katika makazi ya watu na huduma za jamii," alisema Rukia.

Mwakilishi wa Chwaka, Issa Haji Gavu, alisema hatua ya bodi ya vileo kuteua kampuni tatu itasadia kudhibiti uingizaji wa vileo holela pamoja na kudhibiti mianya ya ukwepaji wa kodi. Gavu alisema serikali inapaswa kupongezwa kwa namna inavyosimamia sheria ya vileo kwa vitendo na kuleta faraja kwa wananchi baada ya kuwepo malalamiko mengi ya kero za baa katika maeneo ya huduma za jamii.

Mwakilishi wa Malindi, Mohamed Ahmada Salum, alisema vyombo vya ulinzi na usalama vinapaswa kushirikiana katika kusimamia sheria mpya ya vileo ili kudhibiti vileo vinavyoingizwa kwa magendo na kupoteza mapato ya serikali.

Alisema ziko baa zimeanzishwa katika makazi ya watu au sehemu za huduma za jamii na watoto wa umri wa miaka 18 wanaruhusiwa kuingia wakati ni kinyume cha sheria, mila na utamaduni wa Zanzibar.

Hivi karibuni, Mwenyekiti wa Bodi ya Udhibiti wa Vileo (ZLB), Bwana Khamis Haji, alisema bodi imefanya ukaguzi katika baa 67 kabla ya kuanza kutoa leseni kwa madhumuni ya kuondosha zile ambazo zimekuwa kero katika maeneo ya huduma za jamii, zikiwamo nyumba za ibada.



**JUX**
UKURASA 12



Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE



# #INUKA KITANDANI
# Mshike mkono Profesa Jay arudi jukwaani

MSANII mkongwe wa Bongo Fleva, Joseph Haule, maarufu kama Profesa Jay, bado anapigania maisha yake katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, ambako anapatiwa matibabu.

Profesa Jay anatimiza mwezi mmoja tangu aripotiwe kuwa katika hali mbaya, hata hivyo juhudi sasa zinazidi kushika kasi kuhakikisha msanii huyo ananyanyuka kitandani na kuendelea na shughuli zake.

Juhudi za kumchangia fedha kwa ajili ya kumudu matibabu yake zimeanza, huku mke wake Grace Mgonjo, akithibitisha kuruhusu jambo hilo, kutokana na gharama kubwa ya matibabu inayofikia kiasi cha shilingi milioni nne kila siku.

Hata hivyo, kumekuwepo na malalamiko kutoka kwa wasanii wenyewe kujitenga na kutokuwa na moyo wa kusaidiana pale mmoja wao anapopata matatizo.

Baadhi ya wachambuzi, wanasema ili kuondoa dhana hiyo, ugonjwa wa Profesa Jay, uwe sehemu ya kujisahihisha kwa kujitokeza kwa wingi ili kumsaidia kutoka katika hali hiyo ngumu.

Kulingana na maelezo ya Grace, ni kwamba kiasi hicho cha matibabu ni kikubwa na inahitaji usaidizi kutoka kwa watu mbalimbali ambao walikuwa wakimpenda kutokana na kazi yake nzuri ya kuburudisha pamoja na kuwatumikia wananchi wa Mikumi kama mbunge.

"Kila msanii na wananchi anayeguswa ni lazima kusaidia jambo hili kwani imekuwa kawaida ya wanamuziki kulalamikiwa kutosaidiana katika matatizo sasa ni muda wa kusahihisha," amesema Abdul Shaweji, mkazi wa Kinondoni.

Kulingana na tangazo hilo, michango yote haitapitia kwa mtu mwingine bali itapokelewa na familia kwa niaba yake kupitia namba 0757 919 192 jina Joseph Haule na namba 07715 919192 kwa jina pia la Joseph Haule.

BASI SAWA

## Vaccine ya Simorix yakimbiza




MSANII wa kizazi kipya anayeishi Australia, Simorix The General, amewashukuru mashabiki kwa mapokezi ya wimbo wake mpya , 'Vaccine' ambao ameuachia hivi karibuni.

Simorix, amesema ngoma hiyo yenye maana ya Chanjo ni maalumu kwa wapendanao na umepokelewa vizuri kwa sababu ya ujumbe wake mzuri wa mapenzi.

"Vaccine imeanza kufanya vizuri katika kipindi hiki cha Valentine, ninaongelea penzi kama chanjo naamini kila mtu ana mpenzi wake ambaye ana umuhimu mkubwa kwenye maisha yake," amesema Simorix.

## Sarafina amwagia sifa Mama Samia



MWANAMUZIKI wa bongo fleva, Sarafina Michael, amemwagia sifa Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kutumia sanaa ya muziki kuwakilisha ujumbe wake kwa wananchi.

Sarafina ambaye yuko nafasi ya tano kati ya orodha ya wasanii 20 waliopata tuzo, ameipongeza serikali kupitia wizara husika katika kutekeleza majukumu yake.

"Kwanza naipongeza Serikali ya Rais Samia kwa kufanya kazi kubwa kuinua muziki na kuutumia kama chombo cha kuwasilisha ujumbe wao, hii ni hatua kubwa," alisema Sarafina.



## Jux awaonea huruma warembo wa uswazi

MKALI wa muziki wa R&B, Juma Jux, amesema huwa anapata shida kuanzisha uhusiano wa kimapenzi na wasichana wa kawaida kwa sababu hataki kuwaingiza katika maisha ya kufuatiliwa kila siku.

Amesema katika maisha ya kistaa yana mambo mengi ambayo yanafuatiliwa na watu wengi, hivyo unapoamua kumchukua mtu ambaye hajazoea anapata tabu.

"Sio sitaki kuwa na uhusiano na wanawake wa kawaida, lakini naumia pale ninapoona mtu ambaye hajazoea kufuatiliwa kila siku anaingia katika maisha hayo ghafla," amesema.

## Chikole: Hukumu ya kifo kama mkole

Na Adam Fungamwango

'CHIKOLE' ni filamu moja ya kusisimua, na si hivyo tu, bali ina mafunzo makubwa kwa jamii. Inahusu mahusiano. Mapenzi ni kitu cha ajabu sana ambacho hakuna binadamu yoyote yule ameshawahi kukitolea ufafanuzi unaoeleweka. Yanatesa watu wengi, madaktari, waganga wa kienyeji, wasomi, matajiri na mafukara.

Unaweza kukuta mtu anampenda huyu, lakini anayependwa hamtaki anayempenda. Naye ana mtu mwingine anayempenda, ambaye na yeye pia hamtaki huyo anayempenda, naye akili yake iko kwa mwingine. Huu ni mzunguko ambao bado haujapatiwa jawabu hadi leo.

Imechezwa na kundi la Tumaini Sanaa Group. Inaanzia kwa mfalme Madai wa himaya ya Nanguruwe. Mfalme huyu ana binti yake Chikole ambaye ameondokea kumpenda sana kijana Galawa.

Chimole, kijana mmoja kwenye himaya hiyo, yeye anampenda sana Chikole binti mfalme, lakini ndiyo hivyo, binti amekufa kwa Galawa.

Kuna msichana anaitwa Kalunde anatokea kumpenda Galawa, lakini kijana huyo moyo wake upo kwa binti mfalme.

Kijana wa mfalme aitwaye Mkopi, naye akatokea kumpenda Mwani, dada yake Galawa.

Uhusiano wa ndugu wawili wa Mama Mjane, Galawa na Mwani kuwa na uhusiano wa ndugu wawili wa mfalme, Chikole na Mkopi, ukawa chukizo kwenye himaya hiyo, kwani mizimu ilionekana kukataa. Haiwezekani ndugu wa tumbo moja wa upande mmoja kwenda kuolewa na ndugu moja wa upande mwingine. Ikabidi kila mmoja atafute mchumba mwingine. Hiyo haikuwezekana. Wote wanne waliona ni bora masharti yavunjwe, lakini si kuachana. Tango, Chimela, Tito na Mtanza wanamkamata, kumbaka na kumuua Chikole kwa sababu tu amewakataa.



Mfalme anachukizwa akidhani kuwa Galawa amemuua binti yake. Akaahidi kulipa kisasi. Siku chache baadaye Mwani naye anabakwa na kuuawa na watu hao hao kwa sababu amewasikia wakijisifu.

Mzimu wa Chikole unarejea duniani na kulipiza kisasi na kuwamaliza wote waliombaka na kumuua. Chimela analazimishwa na mzimu aende eneo la hukumu ambako mfalme alikuwa amewakusanya watu wote wa himaya yake kwenye mti mkubwa, akitaka kumuua Galawa.

Alipofika alieleza ukweli wote. Ukweli wote ukadhihirika hapo na Chimela sasa ndiye anayechukua adhabu ya kuuawa badala ya Galawa ambaye sasa alikuwa wameshaanza kupendana na Kalunde aliyemkataa awali.





## Shilole hilo dongo la nani?

MWANAMUZIKI na pia mjasiriamali, Zuwena Mohamed, maarufu kama Shilole, ametumia wimbo mpya wa Zuchu unaoitwa 'Kamwambie' kumpiga dongo Uchebe ambaye ni mume wake wa zamani.

Shilole aliweka video fupi ya wimbo huo katika ukurasa wake wa Instagram, akiwa na mume wake Rommy huku kibwagizo cha wimbo huo kikisikika.

Baadhi ya mashabiki wake walisema ujumbe huo ulimlenga mume wake huyo wa zamani akimtaka kutulia na kwamba hataweza kuachana na Rommy hivi karibuni.

## WAREMBO HAWA HAWACHACHI MDOMONI

Na Adam Fungamwango

WASANII na mastaa wa Kitanzania nao wana mambo. Ni kama binadamu wengine wa kawaida, ukizunguka huku na huko na kukutana nao, na wao pia wana mtazamo na uhuru wao wa kuongea kama mtu mwingine yoyote yule.

Kumekuwa na dhana kwa mashabiki kuwa wao tu ndiyo wana haki ya kuongea, lakini mastaa wakitoa au kusema chochote kama uhuru unavyowaruhusu, wamekuwa wakishambuliwa kwa sababu eti yeye ni maarufu hapaswi kufanya hivyo. Hapana. Nao waachwe wajimwayemwaye kama watu wengine.

Nimepitia kwenye mitandao yao ya kijamii na kukuta wametupia mambo mbalimbali yanayohusu mambo mbalimbali ya kijamii, yanayowasibu, au kukutana nayo mitaani. Wanatahadharisha, kuelemisha na kuburudisha pia kama kawaida yao. Leo nimeweka mastaa wa kike watupu.

**AMBER LULU**

"Halafu wewe acha kudeka, nakapenda kama vile baba Kayumba."

Ni maneno aliyoyaandika Amber Lulu kwenye mtandao wake wa instagram, akiweka pia picha akiwa amemkumbatia msanii Kayumba. Msanii huyo ametoa ngoma aliyoiita 'Halichachi', akishirikiana na Kayumba. Picha hiyo ni moja kati ya matangazo ya ngoma hiyo.

**WEMA SEPETU**

Haitaji utambulisho sana, kwani ni maarufu mno. Kifupi ni Miss Tanzania wa zamani, mwigizaji na mwanamitindo yeye ameandika

"Yaani binadamu bwana, usipofanya wanasema. Ukifanya pia wanasema, sasa sijui nifanye nini, hebu mniache. Haya basi tufanye saba kichwa challenge, maana nimewachoka kwa kweli."

Anaandika huku akiposti video yake fupi akiwa amesuka nywele mtindo wa saba kichwani.

**JENIFER KYAKA ODAMA**

"Kumbuka kuna watu wameumbwa kukupinga tu, haijalishi umefanya mazuri gani, kwao au kwa jamii fulani wao watapinga kuonyesha kwamba ulichofanya sio muhimu. Usilazimishe wakuelewe, songa mbele tu, acha Mungu ashughulike nao." Ni staa wa bongo movie mwenye mvuto anayependwa na wengi, Jenifer Kyaka, jina maarufu la kazi ni Odama. Ameandika hivyo kwenye akaunti yake ya instagram.

**SHAMSA FORD**

Staa mwingine wa bongo movie, Shamsa Ford, yeye ameandika maneno yafuatayo. " Ahsante, samahani, nimekusamehe, nakupenda. Ni maneno madogo lakini yanachukua nafasi kubwa kwenye maisha yetu hapa duniani." Hapa ametoa somo kwa mashabiki wake na jamii kwa ujumla.

**IRENE UWOYA**



Mmoja wa wasanii wa bongo movie mwenye mvuto, Irene Uwoya ameandika hivi "Ujana wako ndiyo utaamua uzeeni ucheze golf au draft." Ameamua kutumia mfano huo, lakini maana yake ni kwamba utakachokifanya ujanani kiwe kizuri au kibaya, ndicho utakachovuna uzeeni. Somo hapa ni kujipanga kabla ya kuwa mzee. Msemo huu unafanana na ule wa 'fainali uzeeni.'




## Kanye West sasa amrudia Mungu

RAPA Kanye West ametumia ukurasa wake wa mtandao wa kijamii kumwomba Mungu amsaidi kuirudisha pamoja familia yake.

Kanye West ameomba hayo wakati akihojiwa na radio moja nchini Marekani, akieleza jambo hilo analiomba lifanyike haraka iwezekanavyo,

"Mungu wangu tafadhali rudisha familia yangu ikae kwa pamoja," ameandika Kanye West.

Msanii huyo na aliyekuwa mkewe Kim Kardashian, walifanikiwa kupata watoto wane North, 8, Saint, 5, Chicago, 4, na Psalm, 2.



## Nelly aponzwa na video ya mrembo

VIDEO fupi ya dakika kadhaa, imemtia hatiani mwanamuziki wa Marekani, Nelly, kiasi ambacho imembidi kujitokeza na kumuomba radhi  msichana anayehusishwa nayo.

Kulingana na ukurasa wa Instagram wa msanii huyo, video hiyo iliwekwa katika ukurasa huo kama kuufanyia promo wimbo wake mmoja 'No Matter What I Do' .

"Nachukua nafasi hii kumuomba radhi binti kijana na familia yake kwa kumuweka wazi katika hili, hii ni video ya zamani ambayo nilihifadhi binafsi na sikupaswa kuweka kwa umma," amesema.

## Kwame, Anica hongera zenu

OKYEAME Kwame na Anica, wanaongoza kuwa mastaa maarufu ambao wamedumu kwa muda mrefu katika uhusiano wa kimapenzi.

Katika ripoti iliyotoka hivi karibuni imebaini Kwame na Anica ambao wao katika ndoa wanaendelea kuishi kwa muda wa miaka 13 bila kuwa na migogoro.

Kapo nyingine ambayo imedumu kwa muda mrefu ni Selly Gal na Praye Tietia ambao wana miaka kumi katika ndoa yao.





## Adele furahia kwani harusi inanukia

MWANAMUZIKI kutoka Uingereza, Adele inadaiwa tayari amevishwa pete ya uchumba na mpenzi wake wa sasa.

Kuvishwa kwa pete hiyo inafuatia kuwepo kwa fununu kwamba msanii huyo ameachana na mpenzi wake Rich Paul.


"Nimefurahi kumaliza onyesho langu wiki iliyopita, pia nina furaha zaidi na pia namtumia Rich ujumbe wa upendo," ameandika.

## Mwigizaji mkongwe amaliza mwendo

MWIGIZAJI mkongwe wa Nigeria, Romanus Amuta, maarufu kama  Natty amefariki dunia.

Kulingana na ripoti msanii huyo wa filamu ameiaga dunia siku ya Jumanne baada ya kuugua kwa muda mrefu.

Natty ambaye kazi yake ya kwanza alifanya katika gazeti la Daily Times, na baadae akajiunga na tasnia ya filamu za Nollywood,



MAKALA

# Makandarasi wa ndani wanapojengewa uwezo kukabili ushindani miradi mikubwa

Na Joseph Mwendapole



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akikagua kazi ya ujenzi wa Mradi wa Bwawa la kuzalisha umeme la Julius Nyerere, katika mto Rufiji mkoani Pwani.

MIONGO kadhaa kazi za miradi ya ujenzi wa miundombinu imekuwa ikifanywa na kampuni kubwa za nje, hivyo fedha nyingi zinakwenda kuzinufaisha nchi wanakotoka.

Hali hiyo imekuwa ikisababishwa na mambo kadhaa ikiwamo ukosefu wa mitaji, mitambo na ujuzi mdogo wa makandarasi wazalendo kumudu kutekeleza miradi mikubwa kama bwawa la umeme la Julius Nyerere, na reli ya Standard Gauge (SGR), ambayo inagharimu trilioni za fedha.

Kuna umuhimu mkubwa wa mikakati kuwekwa kuwawezesha makandarasi wa ndani ambao wanafikia 12,693 kupata uwezo wa mitaji, mitambo ya kisasa na utaalamu wa hali ya juu kwani bila hivyo safari itakuwa ndefu kupambana na kampuni za nje.

Kwa kuona umuhimu wa kuwawezesha makandarasi wa ndani, Bodi ya Usajili wa makandarasi (CRB), imekuwa ikiendesha mafunzo ya kuwajengea uwezo makandarasi hao kwenye mikoa mbalimbali nchini.

Mafunzo hayo yamekuwa yakilenga kuwawezesha kupata utaalamu wa kujua mambo ya kufanya wanapojaza zabuni, mambo ya kuepuka na namna ya kusimamia miradi ya ujenzi kwa ufanisi.

Kwenye mafunzo yaliyofanyika hivi karibuni mkoani Dodoma, makandarasi wa ndani 175 walishiriki mafunzo kuhusu namna ya kutekeleza miradi yaani "Construction Pre-Contract Practices" yaliyolenga kuwasaidia kuandaa zabuni shindani ikiwemo mambo yawapasayo kuzingatia katika mchakato mzima wa kushiriki zabuni.

Mambo mengine waliyofundishwa ni namna ya kutengeneza bei za kazi mbalimbali za ujenzi ili kuwa na bei shindani za zabuni na hatimaye jinsi ya kuwasilisha kitaalamu.

Pia washiriki walielekezwa jinsi ya kutumia mfumo wa kielektroniki wa manunuzi kwa miradi ya Serikali, TANEPS unaosimamiwa na PPRA.

"Mafunzo haya ni muhimu sana kwa kuwa zabuni iliyoandaliwa vizuri ni lazima hatimaye iwasilishwe ndipo iingie kwenye ushindani. Kwa kuwa Mwajiri mkubwa wa makandarasi ni Serikali na Serikali inapokea zabuni kupitia TANEPS pekee, basi umuhimu wa ujuzi wa kutumia TANEPS ni dhahiri mno," anasema Injinia Jere.

Wakati akifunga mafunzo hayo, Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Consolata Ngimbwa, aliwaasa makandarasi kuyachukulia kwa umakini mafunzo hayo kwani ndiyo yatakuwa mkombozi wao kwenye kuongeza ujuzi wao.

Anasema CRB imejitahidi kuandaa mafunzo mengi yakiwemo ya namna ya kuandaa mikataba, kujaza zabuni kielektroniki na namna ya kuwasilisha, hivyo lazima makandarasi wayatumie kuongeza ubora wa kazi zao.

"Kuna mtu anachangia mada kwenye mkutano lakini akitoka hapo getini yote aliyojifunza anayaacha hapo, sasa naomba tuyaishi haya tunayojifunza kwa sababu ni kwa faida yetu sisi wenyewe kukuza biashara hii. Mwezi ujao kutakuwa na mafunzo ya menejimenti na kufanya kazi kwa ubia naomba mhudhurie muongeze ujuzi," anasema

Anasema ni vizuri kuwatumia wataalamu kwenye utekelezaji wa shughuli zao, lakini wanapaswa kutokuwa wategemezi kupita kiasi. Mafunzo hayo yatawaweka sawa na kuachana na utegemezi wa kujaza zabuni na kuendesha kampuni zao.

Anasema kazi za ujenzi ziko nyingi lakini zina ushindani, badala ya kukaa na kulalamika kwamba hawapati kazi wayatumie mafunzo hayo kuongeza ujuzi hasa kwenye kujaza zabuni kielektroniki na kuweka bei halisia.

"Hakuna kazi nyingi kwamba kila mtu atapata, lakini zipo za ushindani na ili uweze kushindana kwenye soko hili ni lazima uwe na ujuzi mkubwa kwenye menejimenti, kujaza zabuni na kusimamia mikataba," anasema

**"Kuna mtu anachangia mada kwenye mkutano lakini akitoka hapo getini yote aliyojifunza anayaacha hapo, sasa naomba tuyaishi haya tunayojifunza kwa sababu ni kwa faida yetu sisi wenyewe kukuza biashara hii. Mwezi ujao kutakuwa na mafunzo ya menejimenti na kufanya kazi kwa ubia naomba mhudhurie muongeze ujuzi," anasema**

Aidha, anasema Serikali imejitahidi kutangaza zabuni nyingi za miradi ya maji na ujenzi wa barabara, makandarasi wa ndani watakaobahatika kuipata wanapaswa kuitekeleza kwa ufanisi.

"Mkifanya vizuri mnajitengenezea njia yenu na ya wengine kuaminiwa ukifanya vibaya unatuharibia biashara hii ya ukandarasi ni nzuri na ya heshima kwa hiyo hakikisheni mnalinda heshima ya kazi yetu kwa kufanyakazi nzuri," anasisitiza.

Katika kuwajengea uwezo makandarasi wazalendo, CRB imekwenda mbali zaidi kwa kuanzisha mfuko wa CAF ambao ni mahsusi kwa ajili ya kuwakopesha makandarasi wazalendo wanapopata mikataba ya zabuni.

Mfuko huo tayari umenufaisha maelfu ya makandarasi wazalendo ambao wamekopa na kufanikiwa kurejesha fedha baada ya kukamilika kwa miradi waliyokuwa wamepata.

Msajili Msaidizi wa (CRB), Injinia David Jere anasema awali makandarasi walikuwa wanaweza kukopa kiasi kisichozidi milioni 50 lakini kwa sasa mfuko umeboreshwa na wanachama wanaweza kukopa hadi Sh milioni 100.

Anasema mtaji wa mfuko uliongezeka kutoka Sh Bilioni 3.87 mwaka 2020 mpaka Sh Bilioni 3.9 mwaka 2021, pia idadi ya wanachama wa mfuko imeongezeka kutoka 1,167 mwaka 2020 hadi kufikia 1,266 kwa mwaka 2021.

"Tunawaomba makandarasi mjiunge na uanachama kwenye mfuko huu kwa sababu mwenye sifa za kukopa ni mwanachama pekee na mtu anapokopa ahakikishe anarejesha fedha ili wanachama wengine waweze kukopa," anasema injinia Jere.

Anasema awali mkopo ulikuwa unatolewa kwa makandarasi wa madaraja flani lakini kutokana na kuendelea kukua CAF sasa inakopesha makandarasi wa madaraja yote bila ubaguzi kwa sharti moja tu mhusika awe mwanachama.

Mmoja wa makandarasi waliohudhuria mafunzo hayo, Jimy Claudia, anapongeza CRB kwa hatua ya kuandaa mafunzo hayo mara kwa mara.

Anasema bila kuwa na mikakati thabiti ya kuwawezesha makandarasi wazawa watabaki kuwa watazamaji wa miradi mikubwa na kuendelea kupata zabuni za ujenzi wa madarasa na vyoo vya shule.

"Hii hatua ya kutujengea uwezo ni uamuzi wa kupongezwa kwani kupitia mafunzo haya makandarasi wanapata uzoefu na ujuzi wa kujaza mikataba na kutekeleza miradi na tunaomba mafunzo haya yawe endelevu ili hatimaye tuweze kushindana na wenzetu," anasema

Twikile Joseph naye anasema halitakuwa jambo la kupendeza kuona makandarasi wazalendo wakiishia kujenga miradi ya gharama za chini huku wageni wakichukua miradi yote mikubwa.

"Tukipata fedha zinabaki kwenye mzunguko wa uchumi wa hapa nchini tofauti na wenzetu ambao wengi wanaweka fedha zao nje ya nchi, hivyo kikubwa tunachoomba serikali kuendelea kutujengea uwezo na nina uhakika tutafika huko waliko wenzetu," anasema

## TULIKOTOKA, TULIKO & TUNAKOELEKEA...

# Zama za mgambo walipokuwa kwenye chati, wanaogopwa, watemi balaa!

## ●Kazi zao: Tanganyika jeki, wakikukimbiza hawakuachi...



**Na Adam Fungamwango**

DUNIA inabadilika na mambo yamebadilika kabisa. Kwa sasa vituo vya polisi vimekuwa vingi mno kiasi kwamba uhalifu mdogo mdogo umepungua kwa kiasi kikubwa tofauti na zamani.

Kwenye miaka ya nyuma kulikuwa na watu fulani wanaitwa magangwe. Huyu anaweza kufanya chochote na kumfanyia mtu chochote na asifanywe lolote.

Mtu anaweza kukabwa mchana peupe na watu wasifanye chochote kutokana na mtu mwenyewe anayefanya hivyo. Ukweli ni kwamba wale magangwe wa zamani walikuwa magangwe kweli. Vipande vya watu, warefu na wenye misuli iliyojengeka. Tatizo lao kubwa walikuwa wanafanya vitu kwa kutumia nguvu zaidi kuliko akili.

Mfano gangwe anaweza kukaa katikati ya njia na kuzuia watu wa upande huu kupita kwenda upande mwingine. Na wa kule nao wasije huku. Atakuwa amevaa 'denglizi', sasa hivi inaitwa 'jinzi', yake kifua wazi tena wakati wa jua kali. Atakaa atasimama hapo masaa matatu jasho linamtoka.

Sasa unajiuliza, anapata faida gani kufanya hivyo? Hakuna. Anachotaka yeye ni kuonyesha watu mamlaka ya nguvu zake tu.

Kutokana na kuwepo kwa watu wakorofi, wenye nguvu, wababe, kutokuwepo na vituo vingi vya polisi kama sasa ilisababisha matukio mengi ya uhalifu ya watu kupigwa, kukabwa na kunyang'anywa vitu mbalimbali kama vilemba, pesa, saa, na mikufu ya dhahabu wakati huo.

Kuna watakaoshangaa kidogo hapo. Ndiyo, zamani vilemba vya akina mama kichwani na saa vilikuwa ni vitu vya thamani na mwizi anaweza kuiba na kwenda kuuza, akapata pesa nzuri tu. Mwingine anaweza kushangaa sijaandika simu ya mkononi. Hazikuwepo. Zilikuwa hazina hata dalili za kuingia nchini.

Labda yupo anayefikiri kuwa mbona hata sasa uhalifu upo, watu wanakabwa, kuvamiwa na kunyang'anywa vitu kama zamani? Ndiyo, kuna utofauti.

Zamani ni gangwe mmoja tu anaweza kufanya hiyo kazi. Nimeeleza hapo juu kuwa moja ya sifa za watu hao mara nyingi ni watu wa miraba minne na wenye nguvu za kutosha. Mmoja tu anaweza kupora hata watu wawili kwa mara moja. Siku hizi hawa wanaoitwa au kujiita vibaka kumpora mnyonge mmoja tu ni lazima wawe kuanzia wawili na kuendelea, tena wakiwa na silaha mkononi.

Magangwe hawa hata kukamatwa kwake ilikuwa kwa mbinde. Watu pekee waliokuwa na uwezo wa kuwakamata magangwe hawa bila shida ni mgambo. Ndiyo walikuwa ni kiboko yao kutokana na kuja kundi, lakini aina yao au staili ya ukamataji. Kwa sasa huwa tunawaona wana mgambo wakiwakamata wafanyabiashara ndogondogo, mama lishe, au wale wanaovunja sheria ya Halmashauri au Jiji.

Na wamekuwa hawaheshimiki sana mbele ya jamii kama askari polisi. Ni kwa sababu kwa sasa hawakamati raia wa kawaida kama zamani. Wale mgambo wa zamani walikuwa wanaogopwa zaidi kuliko askari polisi wa kawaida. Kwa sababu askari polisi wanamafunzo ya ukamataji wa kisheria zaidi tofauti na mgambo ambao walikuwa wakati huo wakifanya kazi zinazofanana na za polisi pia.

Wakati askari polisi walikuwa wakikamata kiweledi zaidi, wao mgambo walikuwa wakimkamata mtu wanavyojua wenyewe. Anaweza kwanza akapigwa ngwala, na mateke juu, halafu anapelekwa kwenye ofisi ndogo za CCM, au zamani ziliitwa 'zoni'. Hizo zilitumika badala ya vituo vidogo vya polisi ambavyo kwa sasa vimetapakaa kila kona nchini.

Wakati askari polisi wakikamata raia mhalifu na kumpeleka kituoni huku akitembea mwenyewe na mkorofi zaidi kupigwa pingu, mgambo wao walimpeleka msobemsobe. Wakati mwingine anaweza akawa anapelekwa huku akipigwa mitama au virungu. Au kukamatwa nyuma ya suruali na kunyanyuliwa juu kidogo kiasi cha kumpa shida mhalifu kutembea, badala yake atatembea kwa vidole. Staili hiyo ikapewa jina na watoto wa mjini wakati ule wakaiita 'Tanganyika Jeki'. Yaani ilifananishwa na jeki za kizamani za kunyanyua magari husussan malori yanapokuwa yanatengenezwa.

Na ole wako ukimbie. Jamaa hawa walikuwa ni hodari wa kukimbia, wanaweza kukukimbiza hadi ukachoka mwenyewe ukasimama kwani, kila kichochoro utakachopita wao wapo tu.

Walisaidia sana kipindi kile kupunguza uhalifu enzi ambazo askari polisi na vituo vidogo havikuwa vingi.

Kutokana na mabadiliko kadhaa kwa sasa mgambo hawaruhusiwi tena kukamata raia wa kawaida, hadi itokee operesheni maalumu, na huwa tunawaona kwa sasa kuwa ni wa jiji, wakishughulika na wanaofanya biashara sehemu zisizoruhusiwa, kuvunja sheria za jiji na mengineyo. Hata hivyo hawajawafikia wale wa zamani, ambao walikuwa watata.

Haya ndiyo maendeleo ambayo yamekuwa yakizungumzwa, kwani kazi hii ya ukamataji raia wameachiwa askari polisi wenye ujuzi wa kazi hiyo, pia kuna vituo vingi vya polisi kwa sasa.

Watuhumiwa wamekuwa wakikamatwa na polisi huku haki zao zikilindwa, tofauti na miaka ile.

Ukiona askari polisi sasa hivi amekamata mtuhumiwa au watuhumiwa wakipelekwa kituoni huku wakizungumza kana kwamba ni marafiki, halafu ukifikiria enzi zile mgambo walivyokuwa wakiwapeleka watuhumiwa 'zoni', unabaki kushukuru na kuona kweli kuna mabadiliko makubwa sana nchini.

**Tuma meseji 0716 350534**



HABARI KIMATAIFA

# Giza lazidi kutanda Ukraine, Marekani yawaonya raia wake

**WASHINGTON,** MAREKANI

RAIS wa Marekani, Joe Biden ametoa tangazo kwa raia wa nchi hiyo wanaoendelea kuishi Ukraine kuondoka haraka kutokana na kuongezeka kwa vitisho vya kuchukuliwa hatua za kijeshi na Urusi.

Biden alisema hatatuma wanajeshi kuwaokoa Wamarekani hao ikiwa Urusi itaamua kuivamia Ukraine.

Alionya kwamba mambo yanaweza kutokea haraka katika eneo hilo na haitawezekana kuwaokoa.

Urusi imekanusha mara kwa mara kuwa na mpango wowote wa kuivamia Ukraine, licha ya kuwa na wanajeshi zaidi ya 100,000 kwenye mpaka wa nchi hizo.

Hata hivyo, nchi hiyo imeanza mazoezi makubwa ya kijeshi na nchi jirani ya Belarus, huku Ukraine ikiishutumu Urusi kwa kuizuia kuingia baharini.

Ikulu ya Kremlin ilisema inataka kuweka mstari mwekundu ili kuhakikisha kuwa jirani yake haingii NATO.

Waziri Mkuu wa Uingereza Boris Johnson, alisema Ulaya inakabiliwa na mzozo mkubwa zaidi wa usalama katika miongo kadhaa huku kukiwa na mvutano.

Mvutano kati ya Ukraine na Urusi umefika kiwango cha hatari baada ya kuwepo hali hiyo kwa miaka mingi, lakini juhudi za kidiplomasia pia zinafanya kazi kwa bidii kutafuta suluhisho la mzozo huo.

Kuna masuala mengi nyuma ya mzozo huo ambao ulianza miongo kadhaa iliyopita na kuhusisha nchi hizo kutoleana macho.

Mizizi ya hatua ya hivi punde kati ya nchi hizo mbili inaanzia Oktoba 2021. Hapo ndipo uwekaji mkubwa wa majeshi ya Urusi kwenye mpaka wa Ukraine ulipoanza.

Ripoti za picha za satellite na kijasusi zimefichua kuwa zaidi ya wanajeshi 100,000 sasa wako karibu na eneo hilo.

Ukraine imeibua wasiwasi juu ya majeshi hayo ya Urusi karibu na mpaka wake, ingawa serikali yake pia ilisisitiza kuwa haiamini kuwa Urusi bado iko katika nafasi ya kuchukua hatua za kijeshi.

Msimamo wa Urusi unaeleza kwamba kutumwa wanajeshi sio tishio kwa Ukraine, na ilisema ina haki ya kufanya chochote inachotaka na jeshi lake ndani ya eneo lake.

Wengine wanasema huenda likawa jeshi kubwa zaidi la Urusi lililopelekwa karibu na Ukraine tangu vita baridi.

"Ukraine inataka kuimarisha usalama wake kwa sababu inahisi shinikizo kubwa kutoka kwa jeshi la Urusi, kwenye mipaka na pia ndani ya eneo lake katika sehemu zinazokaliwa za Ukraine," alisema Orysia Lutsevych, Mkuu wa Jukwaa la Ukrainia Chatham House nchini Uingereza.

Lakini Urusi inaamini kwamba uwezo wa kupeleka wanajeshi kwenye mpaka wake ni haki na uhuru wake.

Suala lingine linalochangia mzozo huo ni kujitanua kwa Nato karibu na Urusi, kiasi ambacho kinaweza kuhatarisha usalama wa taifa hilo kubwa duniani.

"Upanuzi zaidi wa Nato kuelekea mashariki na kupelekwa kwa silaha, ambazo zinaweza kutishia Shirikisho la Urusi, haikubaliki," alisema Waziri wa Mambo ya Nje wa Urusi Sergei Lavrov.

Urusi inapinga vikali uwezekano wa upanuzi wa Nato na inataka hakikisho kwamba Ukraine haitajiunga na Nato. Msimamo huo unashikiliwa na mshirika wake wa karibu China.

**BBC**

## Polisi Nigeria wateketeza chupa za pombe

**KANO,** NIGERIA

POLISI wanaoegemea misingi ya kidini nchini Nigeria, wameteketeza karibu chupa milioni nne za bia katika msako mkali wa pombe.

Chupa hizo zilisagwa ardhini na tingatinga katika mji wa kaskazini wa Kano, mbele ya umati wa watu waliokuwa wakishangilia na kusema 'Mungu mkubwa'.

Mji huo wenye Waislamu wengi uko katika mojawapo ya majimbo kadhaa ya kaskazini mwa nchi hiyo ambayo yamepiga marufuku pombe chini ya sheria ya kiislam iitwayo Sharia.

Bia hizo zilikuwa zimenaswa kutoka kwenye malori yaliyokuwa yakitoka eneo la kusini lenye Wakristo wengi, maofisa walemiambia shirika la habari la AFP.

Polisi wa Sharia, wanaojulikana kama Hisbah, mara kwa mara huharibu pombe na dawa za kulevya zilizokamatwa, lakini tukio hilo la Jumatano lilikuwa kubwa zaidi katika msako mkali unaoendelea.

Maofisa walisema waliviringisha chupa 3,873,163 za bia na aina nyingine za pombe kwenye tingatinga kwenye eneo la wazi kama sehemu ya vita dhidi ya vileo.

Walisema kisha mabaki yalichomwa kwa moto na kuruhusu moto huo kuwaka hadi usiku, kulingana na wanakijiji walioshuhudia.

**BBC**



Magari ya kijeshi ya Urusi yaliyobeba makombora yakiwa katika mpaka wa Ukraine, wakati mazoezi ya kijeshi kati ya nchi hiyo na Belarus yakiendelea. **PICHA: AFP**

## DRC yabaki hatua moja kujiunga EAC

**NAIROBI,** KENYA

JAMHURI ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) imebakiza hatua moja kujiunga rasmi na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), baada ya baraza la mawaziri la eneo hilo kupitisha kujiunga kwake.

Mawaziri hao walipiga kura ya kuunga mkono DRC baada ya kumalizika kwa mazungumzo makali jijini Nairobi, nchini Kenya. DRC inaonekana kama soko muhimu kwa eneo hilo kutokana na kuwa na utajiri wa maliasili.

Baada ya wiki kadhaa za mazungumzo, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo sasa inasubiri tu idhini ya Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, ambao watakutana baada ya wiki chache.

Kuidhinishwa na baraza la mawaziri ni hatua kubwa kwa DRC ambayo iliomba uanachama mwaka 2019.

Hatua hiyo inafuatia baada ya kumalizika kwa majadiliano ambayo yalilenga kuanisha sera za nchi hiyo za kijamii na kiuchumi na zile za EAC, utayari wake na uwezo wake wa kuzingatia sheria za EAC.

Hii ni pamoja na hadhi ya mfumo wa kodi wa DRC na sheria za kimataifa. Kujumuishwa kwa soko la DRC la karibu watu milioni 90 kutapanua soko la EAC kufikia zaidi ya watu milioni 300.

Kukubaliwa kwa nchi hiyo kutaifanya kuwa mwanachama wa saba wa kanda hiyo inayojumuisha Burundi, Kenya, Rwanda, Sudan Kusini, Tanzania na Uganda.

**BBC**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI
INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042,
DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAMBO YA NDANI
IDARA YA UHAMIAJI

## MAOMBI YA URAIA



**BI REHEMA ABDILLAH NASSIR NI RAIA WA KENYA**

Ambaye picha yake imeonyeshwa hapo juu,anaomba uraia wa Tanzania kwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi .Yeye ni raia wa KENYA na Nchi atokayo ni KENYA. Kazi yake /Shughuli zake ni **MEDICAL DOCTOR,** Anuani ya mwajiri wake/shughuli zake ni **JAFFERY CHARITABLE MEDICAL SERVICES.** Ameishi nchini tangu 2017, Pia amewahi kuishi Mikoa/Mikoa ya ……………..., Mtu yeyete mwenye sababu za kupinga mwombaji asipewe uraia, atume taarifa yake ya maandishi iliyosainiwa kwa:

**KAMISHNA MKUU WA UHAMIAJI,**
**S.L.P 512,**
**DAR ES SALAAM.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**FIDES MEDAD ASSENGA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya SUBARU yenye namba ya usajili **T 368 CDV,** Chasis namba **SG5050760,** injini namba **EJ20B947011.** Yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa **DR/MBU/RB/61098/2022**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA

Katika Mahakama ya Mwanzo Kihonda
Wilaya ya Morogoro, Mkoa Wa Morogoro

Usimamizi wa Mirathi……14..2022

KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU JAMILA UWESU MUKHI WA MOROGORO

KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA ABUBAKAR HABIBU UWESU.

## TANGAZO

(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hap o juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 16/02/2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
- Endapo kuna yoyote mwenye wosia na marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia ya narehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika.

**Imetolewa Tarehe 10/02/2022**

WHITE MIRACLES (T) LIMITED

12-02.2022

## NOTISI YA SIKU KUMI NA NNE (14)/TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

KWA IDHINI TULIYOPEWA NA MTEJA WETU PROIN LIMITED TUTAUZA KWA MNADA WA HADHARA DHAMANA ZA MDAIWA SUGU

MNADA UTAFANYIKA MAHALI DHAMANA ILIPO KAMA INAVYOONESHWA KWENYE JEDWALI HAPO CHINI, TUNATOA NOTISI YA SIKU KUMI NA NNE (14) TOKA SIKU YA TANGAZO HILI AMBAYO NI 12-02-2022

| JINA LA MKOPAJI | DHAMANA MAHLI ILIPO | TAREHE YA MNADA | AINA YA DHAMANA |
|---|---|---|---|
| BASELEMA INVESTMENT COMPANY LIMITED P.O.BOX 200 BARIADI, SIMIYU | PROIN LIMITED OFISINI P.O.BOX 1495, PLOT NO 2360/75/C VINGUNGUTI AREA NYERERE ROAD DAR ES SALAAM | 28-02-2022 KUANZIA SAA NNE NA KUENDELEA | GARI NAMBARI T 789 DVR, TOYOTA RAV 4 STATION WAGON RANGI YENKUNDU |

**MASHARTI YA MNADA**
1. MNUNUZI ATALAZIMIKA KULIPA SIKU HIYO HIYO ASILIMIA 25% YA BEI
2. ASILIMIA 75% ITALAZIMIKA KULIPWA NDANI YA SIKU KUMI NA NNE (14)
3. ENDAPO MNUNUZI ATASHIDWA KULIPA 75% ATAPOTEZA MALIPO YAKE YA AWALI YA 25% NA MNADA UTARUDIWA TENA

**KWA MAELEZO ZAIDI PIGA NAMBARI**
**0684-937-219 / 0754-916-444**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**KINGAS KINGS BUSINESS COMPANY LIMITED** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **T 478 BQN,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **MKB/TR/RB/2230/2021**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA MAHALI DODOMA

MAOMBI MADOGO NA 20 YA MWAKA 2021

BAINA YA ERASTO GERVAS KISHE (administrator of the state of the late GERVAS JOSEPH TABU KISHE…………MDAI

DHIDI YA

YOHANA MAKALI NA WENZAKE 6…….WADAIWA

**KWA.YOHANA MAKALO**
**POPOTE ULIPO.**

**YAH:KUITWA:KUITWA SHAURINI**

Kwakuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelelzo yake yameelezwa katika nakala ya maombi ambayo inapatikana katika baraza hili Kwahiyo unatakiwa kuhudhuria katika baraza hili wewe binafsi ,wakili au mwakilishiyeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 23.02.2022 saa 3.00 asubuhi kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi

**ANGALIZO.** kama hukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu,baraza lilithibitisha kuwa umepokea hati ya wito ,baraza linaweza kutoa hukumu dhidi yako

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na lakiri/muhuri was baraza hili leo tarehe 04 ya mwezi February,2022

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe MWANGA WA JAMII

Uza,
Chenye Thamani Kubwa Kwa
Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa
Tupigie 0782253676

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HADITHI

DIANA ni msichana mrembo kwa maana halisi ya urembo. Na mwenyewe alijijua kuwa ni mzuri wa shani. Aliwababaisha, kuwaliza, na kuwatia wazimu wanaume wengi ambao alikutana nao, au hata kupishana tu. Wengi walimkimbilia. Wakamtongoza, kumtaka kimapenzi. Wapo waliotaka kumuoa kabisa. Hata hivyo yeye mwenyewe hakujua ni mwanaume gani anayempenda kwa dhati. Alichojua wengi wanamfuata kama nyuki wafuatavyo ua zuri la waridi. Aliacha muda uongee. Alijua mwisho wa siku atajulikana ni nani anayependa uzuri na urembo wake na nani anampenda kwa dhati. Aliyempenda yeye kama yeye na si urembo wake. Fuatilia mtiririko huu wa riwaya hii kabambe, yenye kusisimua na mafunzo kwa jamii.

# Operesheni Namba Moja-13

Na Adam Fungamwango
(0716 350534)




**“Nakuaminia Jan Japo bado mpaka sasa nakuona ni mjanja mjanja, mtoto wa mjini, lakini hadi kufika sasa ni wewe ndiye unayenipa matumaini. Vinginevyo sijui ningekuwa kwenye hali gani.”**

Akili yake ilijua kabisa kuwa mtu aliyesababisha askari polisi kujua hilo ni Afande Marco ambaye hakutaka kutoa pesa. Akakumbuka maongezi waliyozungumza wakiwa kituoni.

“Mpwa wangu ametekwa na wewe umesikia, wanasema tupeleke kiasi cha shilingi milioni hamsini kwenye daraja la Mfugale pale Tazara, leo usiku saa nane, lakini jamaa wamesema tusiwaambie polisi, vinginevyo watamuua. Usingekuwa mpenzi wake nisingekwambia. Kwa sababu wewe ni polisi, lakini nimelazimika kwa sababu pesa zinatakiwa za kuongezea.” Afande Marco alihabarishwa.

“Unasikia kijana, usiwe muoga kiasi hicho, nashukuru kwa taarifa hiyo. We nenda tu nyumbani usiwe na wasiwasi. Ikifika usiku, pelekeni hizo pesa na sisi kama Jeshi la Polisi tutakuja pale na kufanya kazi yetu ya kuwatia nguvuni, halafu watatueleza aliyetekwa nyara yuko wapi.”

“Lakini afande mchezo unaotaka kuufanya ni wa hatari kwa Diana.” Jan alitahadharisha.

“Yule ni mpenzi wangu mimi, nina uhakika hawatomdhuru na mimi hapa ni mkuu na kituo, nawasiliana na wenzangu kufanya jambo hilo.” Marco alimhakikishia Jan kuwa watekaji watatiwa nguvuni na Diana ataokolewa. Ni mawazo aliyokuwa akiwaza siku alipokutana na Afande Marco.

“Ina maana mzigo bado uko pale pale?” Jan aliuliza.

“Inawezekana au isiwezekane. Nina wasiwasi kama polisi walikwenda pale, wanaweza kuwa wamechukua mzigo huo na kuupeleka kituoni.”

Ken akamtazama Jan na kumuuliza swali “Kama wameuchukua mzigo, shilingi milioni kumi na tano, tutapata wapi pesa zingine za kupeleka? Maana wamenipigia simu na kunitisha hapa, wanasema wanazitaka pesa, kiasi kilekile cha milioni hamsini, lakini safari hii kwenye daraja la Kajima, Jangwani, saa sita usiku.”

“Usiwe na wasiwasi mjomba, hilo suala la pesa niachie mimi. Nitakwenda tena kwa Chala.”

“Atatoa tena kweli?”

“Ni bosi wa Diana, atatoa tu, hata kama itakuwa kwa mkopo.”

“Huoni mjomba kama itakuwa ni hatari tukipata tena pesa nusu kama zile za mwanzo, badala ya milioni hamsini. Hii wametupa onyo, halafu ya pili pesa isitimie, itakuwaje?” Mjomba Ken aliuliza tena.

“Uzuri ni kwamba safari hii polisi hawatojua chochote, mambo yatakuwa mazuri, kuhusu pesa kutimia, ninakwambia hiyo niachie mimi. Na mimi mwenyewe kama kawaida nakwenda kuuweka pale chini ya daraja la Kajima.”

Ken alimtazama Jan kwa mshangao. Alimuona ameshaanza kuwa jasiri. Tangu sakata hili lianze, Jan ndiye amekuwa msaada wake mkubwa. Na kadri muda unavyozidi kusonga mbele, ndivyo anavyoonekana kuwa jasiri na kuliona kama lililomtokea ni jambo la kawaida na si la hatari kama linavyoonekana. Na ndiye anayempa nguvu na kuwa na matumaini ya kumpata tena mtoto wa dada yake, Diana akiwa hai.

“Nakuaminia Jan Japo bado mpaka sasa nakuona ni mjanja mjanja, mtoto wa mjini, lakini hadi kufika sasa ni wewe ndiye unayenipa matumaini. Vinginevyo sijui ningekuwa kwenye hali gani.”

“Usiwe na wasiwasi mjomba, nipo na wewe hadi suala hili litakapomalizika.”

“Nakuahidi, litakapokamilika na binti yangu Diana, mtoto wa marehemu dada yangu akiwa hai, nitakupa zawadi kubwa ambayo hutakaa kuisahau maishani mwako.” Mjomba Ken aliahidi, na kumfanya Jan aangue kicheko kilichochanganyikana na aibu. Mjomba alijua sababu.

******************************

Pamoja na kwamba mbu walikuwa wanamuuma na kufyonza damu yake, lakini alivumilia. Na aliposhindwa kufanya hivyo alipeleka mkono taratibu sehemu ambayo wanamuuma na kuwabana na mkono kwa nguvu kabla ya kuwapukutisha. Kazi hiyo aliifanya kwa muda wa robo saa hivi. Ilikuwa ni ngumu, inayotosha, inayohitaji ujasiri na uvumilivu.

Alikuwa amejificha katikati ya majani marefu yanayoota ndani ya maji au pembeni yake.

Yeye alikuwa pembeni kidogo ya maji. Ni maji ya mto unaopitisha maji ya mto Ng'ombe kuyapeleka kwenye bahari ya Hindi. Ni kwenye daraja la Kajima, Magomeni Mapipa. Saa yake ilimkumbusha kuwa ni saa sita kasoro dakika tano. Tayari dakika kama ishirini alikuwa amezipitisha hapo.

Sauti za chura, na wadudu wanaowakawaka usiku, zilimpa taswira isiyoelezeka. Taswira ya kitu ambacho anasubiri kitokee.

Yapata saa mbili usiku alifika pale akiwa na mkoba wake na kuuweka chini ya daraja hilo. Akaondoka. Akaenda kubadilisha nguo sehemu alipoziweka ambapo hazikuwa mbali sana. Alirudi kwa njia nyingine kabisa, akiambaa na ukingo wa mto. Sehemu ambayo aliamini hakuna mtu atakayeweza kumuona. Alijipachika ndani ya kichaka hicho cha majani marefu yaliyoota ndani na pembeni ya maji yanayopita darajani hapo.

Mfuko wa kulia alikuwa amepachika kisu chake ambacho aliamini kingemsaidia. Mfukoni pia alikuwa na bastola. Ni bastola aliyopewa na mjomba Ken.

Lengo lilikuwa ni moja. Kufa au kupona. Kuua au kuuawa. Alishajitolea kufa kwa ajili ya Diana. Alimpenda sana Diana. Ni wiki ya pili na siku kadhaa yumo mikononi mwa majahili. Walimteka, wakihitaji pesa kiasi cha shilingi milioni hamsini ili wamuachie. Kwanza ilishindikana pesa zilipowekwa chini ya daraja la Mfugale Tazara, sasa wametaka ziwekwe chini ya daraja la Kajima, lile la kwanza kubwa ukitokea Magomeni kwenda Faya.

Ingawa hakumwambia mjomba wake, lakini safari hii alimwambia rasmi Afande Marco kuhusu jambo hilo ili polisi waende aneo la tukio.

Mara ya kwanza alimwambia, lakini kilichotokea ni kwamba watekaji walijua kilichoendelea na hawakwenda kuchukua mzigo walioahidiwa, lakini safari hii alichobadilisha ni muda.

Kwanza alichoshangaa ni kwa nini watekaji walijua kuwa polisi wamepata taarifa na kushindwa kwenda eneo la tukio.

Ndiyo maana safari hii alimwambia Afande Marco kuwa watekaji wameahidi kufika saa tisa usiku kuchukua mzigo huo. Ni saa moja zaidi kama zilizowekwa na watekaji hao daraja la Mfugale.

Aliwadanganya. Wao huku wakisema ni saa sita. Wala hakuwadanganya polisi kwa bahati mbaya.

Alijua huenda polisi na watekaji wote kabla ya kuja pale huwa wanatanguliza wapelelezi wao. Na huenda ndivyo ilivyotokea mwanzo na watekaji wakajua kuwa kuna polisi. Ndiyo maana hii akaweka masaa matatu mbele. Alijua hata kama polisi kupeleleza watakuja, lakini wanaweza kuanza saa saba. Muda ambao watakuwa wamekuja kufuata mzigo wao. Hapo alichohitaji ni msaada wa polisi.

ITAENDELEA JUMAMOSI

HABARI MICHEZO

# BODI YA LIGI KUU YATOA NENO IKIIAMSHA SIMBA

**Na Shufaa Lyimo**

BODI ya Ligi Tanzania imeitaka Simba ambao ndio wawakilishi pekee wa nchi waliobakia katika mashindano ya kimataifa kutumia vyema uwanja wa nyumbani katika mchezo wao wa kwanza wa hatua ya makundi utakaochezwa kesho dhidi ya Asec Mimosas kutoka Ivory Coast.

Simba itaikaribisha Asec Mimosas kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam ikiwa ni mchezo wake wa kwanza wa Kundi D.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Mwenyekiti wa Bodi ya Ligi Tanzania, Steven Mnguto, alisema Simba wanatakiwa wahakikishe wanapata na kubakisha pointi tatu nyumbani ili kuanza vyema kampeni ya kuwania taji la michuano hiyo.

Mnguto alisema wachezaji wanatakiwa kuongeza umakini kwa ajili ya kufanikisha malengo yao ya kupata ushindi na si matokeo mengine.

Alisema anajua mchezo huo unatarajiwa kuwa mgumu na wenye ushindani, lakini bado anawaamini Simba wataendeleza rekodi nzuri wanaposhiriki michuano hiyo wanapokuwa nyumbani.

"Mchezo huo utakuwa mgumu na wenye ushindani, Simba wanatakiwa wafanye juhudi ili wawape Watanzania matokeo mazuri, kwa sababu wao wana faida kubwa kwa kuwa wapo nyumbani," alisema Mnguto.

Mwenyekiti huyo alisema wachezaji wakifuata vyema maelekezo watakayopewa na makocha wao, anaamini ushindi utapatikana na hakuna kitakachowasumbua katika mchezo huo.

Aliongeza Simba inakwenda kukutana na moja ya timu kubwa Afrika hivyo amewataka wachezaji wasiwe na presha ya mchezo bali watulize akili zao.

"Watanzania kwa pamoja tujitokeze kwa wingi uwanjani kuisapoti timu yetu kwani ndio wawakilishi pekee ambao wanashiriki mashindano ya kimataifa kwa sasa, wanapeperusha bendera ya taifa," Mnguto aliongeza.

Alisema kwa mara nyingine bodi inaipongeza Simba kwa hatua hiyo na anaamini nafasi ya kuendelea kuipeperusha vizuri bendera ya Tanzania wanayo.



Wachezaji wa Tiger Queens FC kutoka Arusha wakishangilia katika mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania dhidi ya Yanga Princess iliyochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam juzi. Timu hizo zilitoka sare ya mabao 2-2. **PICHA: MTANDAO**

# Kondo atajwa Mbeya Kwanza

**Na Saada Akida**

ALIYEKUWA Kocha wa KMC FC ya jijini Dar es Salaam, Habibu Kondo, ametajwa ameanza mazungumzo na uongozi wa Mbeya Kwanza ambayo pia inashiriki Ligi Kuu Tanzania Bara, imefahamika.

Mbeya Kwanza wanahitaji kocha kufuatia mwalimu wake, Haruna Harerimana kuondoka nchini hivi karibuni na kurejea kwao Burundi kutokana na matatizo ya kifamilia aliyopata.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mbeya Kwanza, Gideon Ngereza, alisema mpango wao ni kutafuta Kocha Mkuu atakayeweza kuiongoza vyema timu yao lakini bado hawajafikia uamuzi kuwa nani atawafaa.

Ngereza alisema hatua hiyo ya kutafuta kocha mkuu ni kuhakikisha kikosi chao kinaendelea kuonyesha ushindani kama kilivyokuwa chini ya Harerimana.

"Kwa sasa ni mapema kuweka wazi hiyo mipango kwa sababu tuko katika mchakato wa kuangalia nani atatufaa kuwa kocha mkuu, tunahitaji kupata mtu sahihi atakayechukuwa nafasi ya Harerimana," alisema Ngereza.

Kuhusu Kondo, bosi huyo ameweka wazi klabu yake haijafanya mawasiliano yoyote na kocha huyo huku kwa sasa ikiwaamini Mwaka Mwalwisi na Nizar Khalifan ambao ndio wanaliongoza benchi la ufundi kambini jijini.

## Coastal yamkingia kifua kocha Medo

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa Coastal Union umesema hauna mpango wa kuachana na Kocha Mkuu, Melis Medo licha ya kuwapo na malalamiko mbalimbali kutoka kwa baadhi ya wanachama na mashabiki wa timu hiyo ya jijini Tanga, imefahamika.

Katibu Mkuu wa Coastal Union, Rashid Mgweno, aliliambia gazeti hili jana hawaoni sababu ya kuachana na kocha huyo kutokana na kazi kubwa ambayo ameifanya katika kikosi chao.

"Bado tunamwamini kocha wetu, kutokufanya vizuri katika baadhi ya michezo ni kawaida katika mpira, hatuwezi kumfukuza kocha kwa sababu timu haijafanya vizuri, tunaangalia vitu vingi," alisema Mgweno.

Alisema wanachokiangalia kwa sasa ni kuongeza ushirikiano katika benchi la ufundi na kuhakikisha timu yao inafikia malengo waliyojiwekea kwenye msimu huu wa Ligi Kuu ya NBC.

"Ligi msimu huu ni ngumu na kila timu imejipanga vizuri, kama unaona msimu uliopita tulifanya vizuri tofauti na msimu huu tunaahidi kujipanga upya," aliongeza kiongozi huyo.

## Azam FC, Geita Gold majaribuni

**Na Saada Akida**

MASHINDANO ya kuwania ubingwa wa Kombe la FA (ASFC), yanatarajiwa kuendelea leo kwa Azam FC kuikaribisha Baga Friends kwenye Uwanja wa Azam Complex, uliopo Chamazi nje kidogo ya jiji la Dar es Salaam.

Mechi nyingine ya michuano hiyo itakayochezwa leo itakuwa ni kati ya Mbuni FC ya Arusha dhidi ya Geita Gold FC, mchezo utakaopigwa kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha.

Kocha wa Azam FC, Abdihamid Moallin, alisema kikosi chake kipo tayari kwa ajili ya mechi hiyo na wamejipanga kupata ushindi ili wasonge mbele katika michuano hiyo.

Moallin alisema licha ya kucheza na timu ya daraja la chini, lakini hawatawabeza na hivyo wamejiandaa kucheza kwa umakini wakati wote.

"Tumejiandaa vizuri kuhakikisha tunapata matokeo mazuri, tutaingia uwanjani kwa kuwaheshimu wapinzani wetu licha ya kucheza katika ligi ya chini," alisema Moallin.

Alisema ana imani kurejea kwa wachezaji wake waliokuwa katika majukumu ya timu ya Taifa kwenye fainali za Kombe la Mataifa (AFCON), kutaongeza nguvu kwenye kikosi chake.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### RONALDO AANZA KUJIPANGA
MSHAMBULIAJI wa Ureno, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 37, anapanga mazungumzo na wakala wake kuhusu mustakabali wake pale Manchester United baada ya kukatishwa tamaa na maisha pale Old Trafford. ***(Star)***

### RICE HAONDOKI WEST
NYOTA wa England, Declan Rice ambaye analengwa na Chelsea, Manchester United na Manchester City, amesisitiza nia yake ya kushinda mataji na kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 aliwatuliza mashabiki wa West Ham kwa kuelezea uvumi juu ya hatima yake kama "kelele tu". ***(Standard)***

### POGBA MBIVU, MBICHI
PAUL Pogba atalazimika kupungiziwa mshahara wake kama kiungo huyo wa Manchester United na Ufaransa mwenye umri wa miaka 28 kama anataka kuondoka. ***(Mirror)***

### KEPA BADO NJIA PANDA
GOLIKIPA wa Chelsea mwenye thamani ya pauni milioni 72, Kepa Arrizabalaga mwenye umri wa miaka 27 anaweza kuondoka pale Stamford Bridge msimu huu wa joto. ***(Sun)***

### KESSIE ANUKIA BARCA
KLABU ya Barcelona wapo kwenye nafasi nzuri ya kumsajili kiungo wa kati wa AC Milan na Ivory Coast, Franck Kessie msimu huu wa joto. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 pia analengwa na Liverpool. ***(Marca)***

### MANE SASA NJIA MOJA
MSHAMBULIAJI wa Liverpool, Sadio Mane mwenye umri wa miaka 29, yuko tayari kuondoka katika klabu hiyo ya Anfield, huku Barcelona na Real Madrid wakimtaka mchezaji huyo wa kimataifa wa Senegal. ***(Goal, via Mirror)***

### TIELEMANS ASHUKA THAMANI
KLABU ya Leicester City imepunguza dau la kumnasa Youri Tielemans (24), kutoka pauni milioni 60 hadi pauni milioni 35, huku Arsenal na Manchester United wakiwa katika mbio za kumnunua kiungo huyo wa kati wa Ubelgiji msimu huu. ***(Het Nieuwsblad,via Metro)***


### SAKA HALI TETE EPL
KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta amekiri kufuzu kwa Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu kunaweza kuwa muhimu katika kumfunga winga, Bukayo Saka mwenye umri wa miaka ,20 - ambaye anahusishwa na Liverpool. ***(Express)***

### AKANJI KUPOKEA KITITA
MLENGWA wa Manchester United, Manuel Akanji atataka kuongezewa mshahara wake maradufu huku Borussia Dortmund wakiweka bei wanayohitaji kumnunua mlinzi huyo wa Uswisi wenye umri wa miaka 26. ***(Bild, via The Sun)***

### ENRIQUE ATAJWA UNITED
KOCHA wa Hispania, Luis Enrique mwenye umri wa miaka 51, ameibuka kuwa mgombea wa kushitukiza kwenye kibarua cha ukocha wa Manchester United. ***(Star)***

### AZPILICUETA VS CHELSEA
MLINZI wa Hispania, Cesar Azpilicueta anataka kuzungumza na Chelsea kuhusu mustakabali wake, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 akihusishwa na mpango wa kuhamia Barcelona mara mkataba wake utakapokamilika msimu wa joto. ***(Mundo Deportivo)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# POGBA KUJIFUNGA KITANZI MWENYEWE

Ni endapo atakubali mshahara wake kupungua kwa kufanya uamuzi wa...

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United inajiandaa kumpoteza kiungo wake, Paul Pogba bure kwa mara ya pili huku Real Madrid, Paris Saint-Germain na Juventus ni miongoni mwa timu zinazopambana kupata huduma yake.

Pogba inabidi akubali kupunguza kiasi kikubwa cha mshahara wake, ikiwa atataka kuachana na miamba hiyo ya jijini Manchester ili aweze kurahisisha uhamisho wake, baada ya kuitumikia klabu hiyo kwa miaka sita.

Lakini mpaka sasa Pogba hajafanya mazungumzo na klabu yoyote isipokuwa Manchester United kwa ajili ya kuongeza mkataba, lakini cha kustaajabisha ni kuwa hatarajii kusaini mkataba mpya na klabu hiyo, na anahitaji kwenda sehemu nyingine.

Real Madrid, Paris Saint-Germain wako kwenye vita ya kuhitaji huduma yake lakini klabu ya Juventus inapewa nafasi kubwa sana ya kumpata kiungo huyo.

Lakini mshahara wake anaopokea kwa sasa wa pauni 290,000 kwa wiki itakuwa ngumu kwake kujiunga kwa sababu mfumo wa sasa wa Juventus hauwezi kulipa kiasi hicho kwa wiki.

Juventus wanajiandaa kumweka sokoni, Paulo Dybala kwa sababu ya kiasi cha mshahara anacholipwa kwa wiki pauni 225,000 ni kiasi kikubwa kwa mfumo wa mishahara mipya ndani ya Juventus.

LIVE IN PLAY

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 918

MECHI KALI

MANCHESTER UTD
VERSUS
SOUTHAMPTON

1 | 1.65
X | 3.98
2 | 4.92

PIGA *150*87#

Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ

HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
18+

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# ANELKA: MBAPPE ATATUA MADRID



**MADRID, Hispania**

HATIMA ya Kylian Mbappe bado inaendelea kuwa ni mjadala mkubwa kwenye vyombo mbalimbali vya habari na gwiji wa zamani wa Real Madrid, Nicolas Anelka amelezea imani yake kwa mshambuliaji huyo wa PSG ataondoka.

Mkataba wa Mbappe na Paris Saint-Germain unamaliza Juni, mwaka huu lakini pande zote mbili bado hazijafikia makubaliano mapya.

PSG inatarajia kuwakabili Los Blancos hao kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16 huku Madrid wakiwashawishi mabosi wa Real Madrid kumaliza dili na Mbappe mapema mara baada ya dirisha la usajili kufunguliwa.

Anelka alisema: "Ninachoweza kusema ni kwamba kwa ujumla anataka kuondoka."

"Nina imani kubwa Mbappe ataondoka PSG na atakwenda Real Madrid msimu ujao wa Ligi Kuu."

# Bale yuko tayari kuondoka

**MADRID, Hispania**

GARETH Bale tayari anaripotiwa amekubali kuhama kabla ya kumalizika kwa mkataba wake Real Madrid.

Mchezaji huyo raia wa Wales amekuwa na wakati mgumu kwa kukosa muda wa kutosha wa kucheza Real Madrid msimu huu tangu kurejea baada ya kucheza kwa mkopo katika klabu yake ya zamani ya Tottenham msimu uliopita.

Ingawa, sehemu kubwa ya kutokuwapo kwa Bale kumetokana na majeraha, huku akirejea baada ya changamoto iliyomsumbua kwa karibu wiki mbili zilizopita au zaidi.

Baada ya kucheza mechi tatu mwanzoni mwa msimu, Bale alikaa nje ya uwanja kwa miezi kadhaa kutokana na tatizo la mgongo.

Amerejea hivi karibuni lakini ameachwa benchi na kocha Carlo Ancelotti.

Bale bado anaweza kucheza katika miezi ijayo, lakini ni hakika mkataba wake, ambao unamalizika mwishoni mwa msimu huu, hautaongezwa tena.

Na kwa mujibu wa El Nacional, mchezaji huyo tayari amekubali kusaini mkataba wa awali na Tottenham.

Inadaiwa Bale atarejea Spurs kwa mara ya tatu ukiwa ni mkataba wa mwisho wa maisha yake ya soka.

Ripoti hiyo inadai Bale alikubali mpango huo miezi mitatu iliyopita.



HABARI MICHEZO


,137,180

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 12/02/22 | 18:00 | Brentford vs Crystal Palace | 2.60 | 3.09 | 2.84 |
| 02. 12/02/22 | 18:00 | Peterborough vs Preston | 2.75 | 3.15 | 2.51 |
| 03. 12/02/22 | 18:00 | Reading vs Coventry | 2.79 | 3.19 | 2.45 |
| 04. 12/02/22 | 18:00 | Birmingham vs Luton Town | 2.81 | 3.15 | 2.46 |
| 05. 12/02/22 | 18:00 | Nottingham vs Stoke City | 2.31 | 3.14 | 3.04 |
| 06. 12/02/22 | 18:15 | Villarreal vs Real Madrid | 2.74 | 3.32 | 2.54 |
| 07. 12/02/22 | 18:15 | Perugia vs Frosinone | 2.40 | 3.14 | 2.90 |
| 08. 12/02/22 | 20:00 | Napoli vs Inter | 2.81 | 3.41 | 2.44 |
| 09. 13/02/22 | 15:00 | Sheffield Wed vs Rotherham | 2.79 | 3.13 | 2.49 |
| 10. 13/02/22 | 16:00 | Alaves vs Valencia | 3.04 | 3.24 | 2.36 |
| 11. 13/02/22 | 18:00 | Real Oviedo vs Huesca | 2.46 | 3.15 | 2.81 |
| 12. 13/02/22 | 19:00 | Kasimpasa vs Alanyaspor | 2.61 | 3.30 | 2.56 |
| 13. 13/02/22 | 19:30 | Leicester vs West Ham | 2.85 | 3.45 | 2.38 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 12/02/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:30 | 3822 | Manchester Utd vs Southampton | 1.65 | 3.98 | 4.92 |
| 15:30 | 4731 | Huddersfield vs Sheffield Utd | 3.15 | 3.25 | 2.20 |
| 16:00 | 3290 | Al Hilal Riyadh vs Al Ahly Cairo | 1.98 | 3.34 | 3.38 |
| 16:00 | 5238 | Cadiz CF vs Celta Vigo | 3.70 | 3.35 | 2.04 |
| 16:00 | 5765 | Bloemfontein Celtic vs Cape Town City | 2.50 | 2.79 | 2.93 |
| 17:00 | 3984 | Lokomotiva Zagreb vs Istra | 1.73 | 3.71 | 3.95 |
| 17:00 | 4670 | Lazio vs Bologna | 1.71 | 3.95 | 4.50 |
| 17:30 | 1180 | VfL Bochum vs Bayern Munchen | 9.98 | 6.98 | 1.22 |
| 17:30 | 1877 | Greuther Furth vs Hertha BSC | 2.88 | 3.33 | 2.39 |
| 17:30 | 4944 | Monchengladbach vs Augsburg | 1.65 | 4.08 | 4.67 |
| 17:30 | 5023 | Eintracht Frankfurt vs VfL Wolfsburg | 2.21 | 3.40 | 3.15 |
| 17:30 | 5104 | SC Freiburg vs Mainz | 2.13 | 3.38 | 3.33 |
| 18:00 | 1219 | Blackpool vs Bournemouth | 3.72 | 3.38 | 1.94 |
| 18:00 | 1644 | Watford vs Brighton | 3.59 | 3.19 | 2.14 |
| 18:00 | 1840 | Barnsley vs QPR | 3.59 | 3.35 | 1.99 |
| 18:00 | 2039 | Motherwell vs Aberdeen | 2.75 | 3.04 | 2.46 |
| 18:00 | 2645 | Millwall vs Cardiff | 2.27 | 3.10 | 3.15 |
| 18:00 | 3298 | Brentford vs Crystal Palace | 2.55 | 3.10 | 2.90 |
| 18:00 | 3546 | Everton vs Leeds | 2.22 | 3.61 | 3.00 |
| 18:00 | 3716 | Peterborough vs Preston | 3.33 | 3.33 | 2.09 |
| 18:00 | 3718 | Birmingham vs Luton Town | 2.81 | 3.15 | 2.46 |
| 18:00 | 4388 | Hull City vs Fulham | 5.09 | 3.67 | 1.64 |
| 18:00 | 4622 | Middlesbrough vs Derby | 1.62 | 3.67 | 5.29 |
| 18:00 | 4673 | Reading vs Coventry | 3.48 | 3.38 | 2.01 |
| 18:00 | 5450 | Partick Thisle vs Dundee Utd | 2.89 | 3.04 | 2.35 |
| 18:00 | 5955 | Nottingham vs Stoke City | 2.32 | 3.13 | 3.03 |
| 18:15 | 4682 | Villarreal vs Real Madrid | 2.54 | 3.39 | 2.69 |
| 18:15 | 4801 | Eupen vs KAA Gent | 4.64 | 3.85 | 1.67 |
| 18:30 | 3295 | Sporting Braga vs Pacos Ferreira | 1.39 | 4.53 | 7.48 |
| 19:00 | 4496 | Kaizer Chiefs vs TS Galaxy FC | 1.49 | 3.66 | 6.36 |
| 19:00 | 5507 | Galatasaray vs Kayserispor | 1.77 | 3.64 | 4.23 |
| 19:00 | 5860 | Montpellier vs Lille | 3.02 | 3.47 | 2.24 |
| 19:30 | 2094 | Chelsea vs Palmeiras | 1.63 | 3.66 | 4.72 |
| 20:00 | 4296 | Banik Ostrava vs Teplice | 1.43 | 4.72 | 6.62 |
| 20:00 | 4835 | Napoli vs Inter | 2.69 | 3.39 | 2.54 |
| 20:30 | 1190 | OH Leuven vs Cercle Brugge | 2.86 | 3.36 | 2.34 |
| 20:30 | 1383 | Mechelen vs Oostende | 1.81 | 3.81 | 3.86 |
| 20:30 | 1889 | Norwich City vs Manchester City | 13.24 | 6.53 | 1.20 |
| 20:30 | 3640 | Rayo Vallecano vs Osasuna | 2.20 | 3.16 | 3.46 |
| 20:30 | 4655 | Annan Athletic vs Rangers | 27.01 | 10.61 | 1.03 |
| 20:30 | 5770 | Bayer Leverkusen vs Stuttgart | 1.41 | 4.98 | 6.37 |
| 20:45 | 4020 | Groningen vs Fortuna Sittard | 1.92 | 3.43 | 3.73 |
| 20:45 | 5079 | Cambuur vs PEC Zwolle | 2.37 | 3.34 | 2.80 |
| 21:00 | 5105 | Benfica vs Santa Clara | 1.26 | 5.52 | 9.86 |
| 22:00 | 1094 | Vitesse Arnhem vs PSV Eindhoven | 4.33 | 3.78 | 1.71 |
| 22:30 | 4690 | St. Gallen vs Servette Geneva | 2.61 | 3.40 | 2.51 |
| 22:45 | 1782 | Zulte Waregem vs Anderlecht | 5.92 | 4.44 | 1.47 |
| 22:45 | 4979 | Torino vs Venezia | 1.49 | 4.28 | 6.37 |
| 23:00 | 1067 | Lyon vs Nice | 1.91 | 3.69 | 3.69 |
| 23:00 | 4947 | Atletico Madrid vs Getafe | 1.44 | 4.18 | 7.77 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# MRADI WA KITUO CHA TFF KIGAMBONI MAMBO SAFI

**Na Mwandishi Wetu**

UJENZI wa kituo cha Michezo cha Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) uliopo katika eneo la Kigamboni jijini Dar es Salaam, upo kwenye hatua za mwisho, imefahamika.

TFF inajenga vituo vya michezo Kigamboni na Mnyanjani jijini Tanga na vinatarajiwa kumalizika kwa pamoja mwishoni mwa mwezi huu.

Akizungumza na wahariri wa habari za michezo jana, Rais wa TFF, Wallace Karia, alisema baada ya kukamilika kwa ujenzi huo, ofisi ya Katibu Mkuu wa shirikisho hilo itahamia Kigamboni kabla ya ofisi nyingine kufuatia Juni, mwaka huu.

"Februari 26 Katibu atahamia hapa (Kigamboni), baadaye mwezi wa sita ofisi nyingine zitahamia pia maana pale Karume (ofisi za sasa za TFF) tutavunja na kufanya tena ujenzi, " alisema Karia.

Uwanja huo mbali na majengo ya ofisi pia utakuwa na hostel, na viwanja viwili kimoja chenye nyasi bandia ambazo tayari zimeshawasili na kingine nyasi za halisi.

Kwa mujibu wa Injinia wa mradi huo, Yasinta Wilbert, kuhusu uwanja wenye nyasi za kuotesha wenye ukubwa wa mita 109 kwa 73 unaojengwa Kampuni ya Group Six International utakuwa tayari kutumika ifikapo Juni, mwaka huu.

Alisema uwanja huo utapandwa mbegu za majani aina ya Bemuda kutoka Afrika Kusini.

Injinia huyo alisema, licha ya viwanja, kampuni yake inatarajia kukabidhi majengo ifikapo Machi, na hapo ndio viwanja vitakamilishwa.

Aliongeza majengo ya ofisi, hosteli za timu za Taifa za wakubwa na wenye umri mdogo yamekamilika kwa asilimia 100.




Baadhi ya wachezaji wa Simba Queens ya jijini Dar es Salaam wakiwa wamepozi kambini kwao baada ya kumaliza mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania hivi karibuni. Simba Queens ndio mabingwa watetezi na vinara wa ligi hiyo yenye timu 12. **PICHA: SIMBA SC**

# Lwanga kamili kuikabili Asec

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO wa kimataifa wa Simba Mganda Thadeo Lwanga, yuko fiti kuivaa Asec Mimosas katika mechi ya kwanza ya hatua ya makundi ya mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Hata hivyo wakati Lwanga akirejea kikosini, winga, Hassan Dilunga yuko katika hatihati ya kucheza baada ya kupata majeraha mazoezini jana.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, ameliambia gazeti hili jana maandalizi ya mechi hiyo yamekamilika na benchi la ufundi limepata faraja baada ya kurejea kwa Lwanga ambaye alikuwa majeruhi tangu Oktoba, mwaka jana.

"Lwanga kwa sasa yupo fiti na anaweza kucheza mechi ya Jumapili inategemea na Kocha Mkuu, Pablo Franco atakavyoona. Inaweza akaona bado hajawa na utimamu wa mwili kucheza mechi hiyo, au atamwingiza kipindi cha pili, au pia akamwanzisha kwenye mechi hiyo kwa sababu tayari amepona ana amefanya mazoezi kwa muda mrefu na wenzake," alisema Ally.

Aliongeza Dilunga naye alipata maumivu akiwa mazoezini, lakini bado wanasubiria majibu ya vipimo vya madaktari ili kufahamu hatima yake kuelekea mchezo huo.

Nyota wengine watakaokosekana katika mchezo huo wa Kundi D ni pamoja na Kibu Denis ambaye pia bado ni majeruhi na Clatous Chama ambaye kanuni hazimruhusu kucheza mechi hiyo kwa sababu tayari aliitumikia RS Berkane ya Morocco katika michuano hiyo ya kimataifa msimu huu.

# Michezo

Jumamosi Februari 12, 2022

Nipashe


UKURASA 21




**Pogba kujifunga kitanzi mwenyewe**




Magolikipa wa Yanga, Djigui Diara (kushoto) na Aboutwalib Mshery, wakipozi kabla ya kuanza mazoezi ya kujiandaa na mechi ya Kombe la FA dhidi ya Biashara United itakayochezwa Jumanne kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

# SIMBA SC, YANGA MAWINDO TOFAUTI

## Mnyama asisitiza ameimarika wakati Nabi akiichimba mkwara Biashara...

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

WAKATI Simba ikisema iko tayari kuanza vyema mechi yake ya hatua ya makundi ya mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Asec Mimosas, Yanga imejipanga kuichapa Biashara United na kusonga mbele kwenye michuano ya Kombe la FA.

Simba itaikaribisha Asec Mimosas kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam huku Biashara United ikiwafuata Yanga katika dimba hilo Jumanne usiku.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Simba, Pablo Franco, alisema ameendelea kutengeneza timu yake baada ya kuona ubora wa wapinzani wao na anaamini mbinu mpya alizowapa zitawajenga na kuwafanya waingie uwanjani wakiwa imara zaidi.

Pablo alisema amepata nafasi ya kuwasoma wapinzani wao na kufahamu ubora wao katika kila idara ikiwamo safu ya ushambuliaji inayoonekana ina uchu wa kufunga magoli lakini pia wakiwa imara kwenye ulinzi.

"Kiufupi tumefanyia kazi mapungufu yetu kwanza yaliyojitokeza katika mechi zilizopita na kuandaa timu ya ushindani ili kukabiliana na wapinzani wetu, kazi kubwa ni kuendelea kuimarisha safu yangu ya ushambuliaji kwa kuwataka mastraika kuongeza utulivu na umakini, kwa sababu mechi zilizopita tulipata nafasi nyingi ambazo tulishindwa kuzitumia," alisema Pablo.

Aliongeza amewaambia wachezaji wake hawatakiwi kuridhika na matokeo ya nyuma kwa sababu wanaanza safari nyingine na kuhakikisha wanafanikiwa katika malengo yao.

"Mashindano yoyote hakuna timu rahisi, Asec wako vizuri na wanaongoza ligi nchini kwao, tutaingia na nidhamu ya hali ya juu na tahadhari kubwa kuhakikisha tunaenda kutafuta pointi tatu muhimu katika mchezo wetu," alisema Pablo.

Kwa upande wa uongozi, Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano, Ahmed Ally, alisema kila kitu kimeenda vizuri na kilichobakia ni kazi ya uwanjani.

Kuelekea mchezo wa Kombe la FA, Kocha Mkuu Yanga, Nesreddine Nabi, alisema 'anapiga jiwe moja' na kutaka kuuwa ndege wawili kwa kufanya maandalizi ya mechi ya hatua ya 16 bora dhidi ya Biashara United, lakini pia kwa mchezo wa Ligi Kuu Tanzania unaofuata ambao wataifuata Mtibwa Sugar huko Turiani, Morogoro.

Nabi alisema mechi mbili hizo zilizoko mbele yao zina ushindani na anahitaji kupata matokeo chanya na kuendelea kujiimarisha kwenye mbio za kuchukua mataji.

"Hii ni mechi muhimu kwetu kwa sababu tunahitaji kutwaa ubingwa wa michuano hii, kufikia huku lazima tupambane tushinde kila mechi, lakini mechi hii ni maandalizi ya mechi yetu ijayo ya ligi, bado tunasafari ndefu, pamoja na kuongoza na ligi lakini bado hatuna uhakika wa ubingwa kwa sababu ligi ni mbio ndefu," alisema Nabi.

Alisema anatambua ligi imekuwa na ushindani mkubwa na hakuna mwenye uhakika wa kutwaa ubingwa hadi sasa hivyo anawataka wachezaji wake kupambana katika kila mechi watakayocheza.

"Nimepata nafasi ya kuzungumza na wachezaji wangu na kuwakumbusha suala la kujituma, kucheza kwa ushirikiano, nina matarajio makubwa wachezaji wangu watazingatia hayo kwa ajili ya kufikia malengo yetu," alisema Nabi.

# Karia afunguka siri wachezaji kuchoka haraka

**Na Mwandishi Wetu**

UBOVU wa viwanja vinavyotumika katika mchezo wa soka nchini umetajwa kuwa ni moja ya sababu inayochangia wachezaji wa Kitanzania kutocheza kwa muda mrefu, imeelezwa.

Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia, alisema hayo jana alipokutana na wahariri wa habari za michezo walipotembelea mradi wa shirikisho hilo wa kituo cha michezo Kigamboni Dar es Salaam na baadaye Mnyanjani, Tanga.

Kituo cha Kigamboni kinatarajiwa kuwa na viwanja vya nyasi bandia na nyasi halisi na ujenzi wake umekaribia kukamilika.

"Tutakuwa na viwanja vizuri pia, viwanja vyetu ni vibovu sana unajua, unaweza kukuta mchezaji ana uwezo wa kucheza kwa miaka 20 lakini anaishia miaka 10 au mitano kutokana na kupata majeraha yanayowalazimisha kukaa nje ya uwanja mapema... mkipata nafasi zungumzeni na watu wa tiba za wachezaji watawaambia.

"Lakini kingine kinachoumiza sana wachezaji wetu nao ni ndondo, sasa kukiwa na viwanja vizuri hata ndondo nazo zitachezwa kwenye viwanja vizuri, hawataumia wachezaji," Karia alisema.

Kiongozi huyo alitumia nafasi hiyo kuwaasa wachezaji waepukane na tabia ya kucheza ndondo kwenye viwanja vibovu ili kutohatarisha afya zao.

Aliongeza wachezaji wengi wanapata majeraha makubwa katika mechi za ndondo baada ya kucheza katika viwanja visivyo na sifa.

"Viwanja katika mradi huu wa Kigamboni vikikamilika, tutapunguza idadi ya uhaba wa viwanja, baadhi ya timu zinaweza kuomba kucheza katika viwanja vyetu na sisi tutaruhusu kwa masharti fulani na ninaamini itasaidia kupunguza baadhi ya changamoto," alisema Karia.

Aliongeza nia ya TFF ni kuiona Tanzania ikiwa na idadi kubwa ya viwanja na kuiomba serikali isaidie kufanikisha hilo katika kila mkoa.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >